KCSE PREDICTOR

SET 1

KISWAHILI

A SERIES OF KCSE PREDICTION KISWAHILI QUESTIONS!

FOR MARKING SCHEMES

CONTACT 0705525657

(PREDICTOR TRIALS 1-10)

MR ISABOKE 0705525657

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 1

KISWAHILI
102/1
KARATASI YA KWANZA
Muda: Saa 1 ¾

MASWALI

1. Lazima

   Wewe ni mhariri wa Gazeti la mwanzo mpya. Andika Tahariri kuhusu umuhimu wa vyama vya wanafunzi shuleni. (alama 20)

2. Uhuru unaopewa Vijana leo katika nchi yetu una hasara nyingi kuliko faida. Jadili. (alama 20)

3. Andika insha itakayodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Adhihakiye kovu hajaona jeraha. (alama 20)

4. Andika kisa kitakachoanza kwa maneno haya: Nilisimama kama ilivyotuamuru sauti nzito ya kutisha,huku nikijikuta na kujawa mawazo tete ya kuhamia sehemu nisiyoifahamu…..(alama 20)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 1

102/2

KISWAHILI
Karatasi ya 2

LUGHA

Muda: Saa 2 ½

1. **UFAHAMU: (Alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Gari lake kuukuu lilikuwa linapambana na barabara yenye mashimo yaliyoshiba na kutapika maji ya mvua ambayo sasa ilikuwa inaanza kupusa. Japo daima alipambana na usukani kunako mashimo haya barabara iliyosakafishwa nayo ikahitimu? Magurudumu haya yaliyong'ara kama upara wa shaibu aliyekula chumvii hadi ikamwogopa yangetii uelekezi wake? Mara ngapi gari hili limetaka kumwasi barabarani? Haya yalikuwa baadhi ya maswali yaliyompitikia akilini. Hakujitakilifu kutaka **kuyapa mji** maana mara ile mawazo yake yalitekwa na kubwagwa katika nchi ya mbali – nchi ambayo sasa aliiona kama sinema akilini mwake.

Alipofika nyumbani aliliegesha gari lake na kufululiza ndani. Siku mbili zilikuwa zimepita akiwa pale kazini. Madaktari kama yeye hawakuwa wengi. Alikuwa miongoni mwa madaktari wenye ujuzi katika hospitali hii ya kitaifa. Wenzake wengi walikuwa wamehamia ughaibuni walikokwenda kutafuta maisha. Mshahara wao wa mkia wa mbuzi uliwasukuma na kuwatema nje ya nchi yao. Wengi wa waliohamia ng'ambo waliona vigumu kubaki katika ajira ambayo kivuno chake kilishindwa kumvusha mtu hata nusu ya kwanza ya mwezi. Malalamishi ya kulilia ujira wa heshima yaligonga kwenye masikio yaliyotiwa zege. Na kweli wanavyosema, mwenye macho haambiwi tazama. Basi walitazama hapana pale wakaona penye mianya ya matumaini,nao wakaiandama.

Hadi leo hii hamna la mno lililofanyika. Ndiyo maana Daktari Tabibu anarudi nyumbani tangu kuingia kazini hiyo juzi alfajiri. Hafanyi kwa kuwa katosheka,maana pia yeye an dukuduku. Ana shaka ya mustakabali wake ikiwa mazingira ni haya kumsoza,maana umri nao unazidi kumla. Japo anatia na kutoa,mizani ya hesabu yake imeasi ulinganifu.

Daktari Tabibu ni mfungwa. Ametekwa na kuzuiwa kwenye kipenda na kuchukia mambo. Ni kama mti uliodumaa. Anatami barabara nzuri lami. Anatamani mshabara wa kumwezesha kukidhi mahitaji yake ya kutimiza majukumu yake ya kimsingi. Jana amesema na rafiki yake

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

aliye ng'ambo kwa simu ambayo sasa imetulia mkabala naye. Ingawa mwenzake huyu alikuwa mchangamfu na kumdokolea hali ya maisha ya kuridhisha kule ugenini kama vile wanataaluma kuenziwa,yapo vilevile yaliyomtia unyonge moyoni. Upweke ndio ulimtia **fukuto** kuu. Licha ya hela zote hizo za kupigiwa mfano,watu hawana muda wa kutembeleana nakujuliana hali au hata kukutana tu mkahawani wakashiriki mlo. Eti ni kila mtu na hamsini zake. Halafu ipo changamoto ya hali ya hewa. Baridi ya ng'ambo haifanyi mzaha katika kumtafuna mtu. Ni hali tofauti na ile aliyoizoea.

Daktari Tabibu alizitia kauli za rafiki yake kwenye mizani ya moyo wake. Akawaza ikiwa kweli si bora kulemazwa na mzizio ugenini badala ya kuishi katika kinamasi cha kuumbuliwa nyubani. Kisha punde lilimjia wazo la marehemu nyanyake na wengine kama yeye waliofadhili masomo yake kupitia kwa serikali ya njia ya kodi. Je si usaliti huu?Vipi aikimbie nchi kabla ya kuihudumia ilhali imemjenga hadi kuwa daktari? Na je wafanyakazi wake wa nyumbani watakwenda wapi? Atawaambiaje kuwa sasa hahitaji huduma zao kwa kuwa anakimbia nchi yake?

Mawazo yake yalikatizwa na simu iliyolia na kumshtua. Alipoitazama aliiona imeng'ara kwa mwangaza ulioweka wazi jina la mpigaji. Alifahamu kuwa leo hii tena dharura nyingine ilikuwa inamwalika hospitalini. Hapo ndipo alipoiinua ile simu tayari kusema na mwenzake upande wa pili.

"Haloo!" sauti nyororo kutoka upande wa pili iliita.

"haloo!"

"Naam!Dharura nyingine tena daktari. Unaombwa kuokoa maisha mengine tena!"

"Haya. Ila mwanzo nitahitaji kujimwagia maji," na pale pale akaikata ile simu.

Daktari Tabibu aliingia hamamuni huku kajifunga taulo kiunoni tayari kuoga. Aliyafungulia maji lakini ule mfereji uligoma kutapika maji. Ulikuwa umekauka kabisa. Daktari Tabibu aliduwaa pale. Aliufunga ule mfereji kabla ya kuiaga bafu.

Maswali

(a). Eleza sababu nne zinazowafanya wataalamu kuhamia nchi za nje. (Alama 4)

……

……

……

……

……

……

(b). “Hakuna masika yasiyokuwa na mbu” Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hali ya waliohamia ng;ambo. (Alama 3)

……

……

……

c). Fafanua athari tatu zinazoikumba nchi ya msimulizi kutokana na uhamiaji ng’ambo wa wataalamu (alama3).

……

……

……

(d). Eleza mchango wa teknolojia kwa kurejelea kifungu. (Alama 3)

……

……

……

(e).Eleza maana za msamiati ufuato kulingan na taarifa. (Alama 2)

(i). Kuyapa mji

……

……

(ii). Fukuto

……

2. **UFUPISHO (Alama 15)**

Wakenya walipolipata katiba mpya waliidhinisha mfumo wa ugatuzi. Katika mfumo huu,mamlaka ya serikali kuu katika uongozi,usimamizi na utumiaji wa rasilimali za nchi hupunguzwa. Kiasi Fulani cha mamlaka hutwaliwa na maeneo ya ugatuzi. Suala hili halikuzingatiwa katika katiba ya awali ambapo mamlaka yote yalikuwa mikononi mwa serikali kuu. Kutokana na upana na wingi wa maeneo,iliiwia vigumu serikali kuu kuhakikisha kwamba kulikuwa na usawa wa kimaendeleo katika sehemu nchini.

Kwa mujibu wa katiba mpya,serikali kuu haina budi kuyasidia maeneo yote ya ugatuzi ili yaweze kujinyanyua kiuchumi na kuboresha hali za maisha za wakazi wake. Vilevile ni jukumu la kila eneo la ugatuzi kuweka mikakati madhubuti ili kuchunguza na kubainisha rasilimali zote katika maeneo husika. Hili litasaidia kufumba rasilimali ambazo zinaweza kuchangia katika ustawishaji wa maeneo haya. Maeneo haya pia yanatakiwa kutafuta mbinu zitakazofanikisha uzalishaji na utumiaji wa rasilimali hizi kwa njia endelevu. Mojawapo ya mbinu hizi ni uongezaji thamani katika rasilimali yoyote inayozalisha kwenye eneo mahususi.
Maeneo mengi ya ugatuzi nchini humu yanategemea kilimo cha ufugaji kama mhimili wa uchumi. Licha wenyeji kikamilifu. Aghalabu kuwa nguzo,kilimo hiki hakijawahi kupigiwa

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

darubini vizuri kwa lengo la kukiimarisha ili kiwanufaishe wenjeji kikamilifu. Aghalabu wafugaji wengi huandama mbinu za jadi za ufugaji ambazo haziwahakikishii ongezeko la mapato. Isitoshe,wafugaji hawa wanakabiliwa na tatizo katika soko la mifugo ambapo wengi hupunjwa na matapeli. Pamoja na haya,baadhi ya wakazi huuza mifugo nje ya nchi wakiwa wazimawazima bila kuwazia matokeo ya kitendo hiki. Si ajabu kuwaona ng'ombe, ngamia,mbuzi, na kondoo wakipakiwa kwenye malori na kusafirishwa nje ya nchi. Ukweli ni kwamba jambo hili ni hatari sana,si kwa uchumi wa maeneo husika tu,bali pia kwa Kenya kwa jumla . Hii ni kwa kuwa walionunua mifugo wazimawazima wanaweza kuhiari kutowachinja na badala yake kuwatumia kama mbegu kwani baada ya muda huenda wanaonunu mifugo wakijitosheleza na kukosa kununua mifugo wengine. Hali ikiwa hivyo, maeneo yaliyotegemea soko hili huenda yakalipoteza taratibu,na bila shaka kupoteza natija inayotokana na soko lenyewe

Ili kudhibitisha hali hii,itakuwa bora ikiwa viwanda vya kuchinjia mifugo na kupakia nyama vitajengwa katika maeneo haya ya ugatuzi. Hili litawawezesha wakazi kuuza nyama badala ya kuuza mifugo wazimawazima. Fauka ya hayo maeneo haya yatajikinga dhidi ya kupoteza bidhaa zinazotokana na mifugo. Hizi ni kama vile ngozi, kwato na pembe ambazo bila shaka zina natija kuu. Ngozi kwa mfano,ni bidhaa muhimu sana katika sekta ya utengenezaji wa mavazi na mifuko. Viwanda vinavyotumia ngozi kama malighafi vikijengwa katika maeneo haya,wakazi wake watanufaika si haba. Madhalani,viwanda vya kutengenezea viatu,mishipi,mifuko na nguo vikianzishwa,wawekezaji watalazimika kuanzisha viwanda vingine tegemezi. Kathalika,ni dhahiri kwamba bidhaa zinazotokana na ngozi huhitaji kutiwa nakshi. Kuanzishwa kwa viwanda hivi basi kutazua haja ya kuanzishwa kwa viwanda vingine vya kutengeneza rangi,pamoja na maduka ya kuuza bidhaa zenyewe. Isitoshe,gundi ya kugandisha bidhaa hizi itahitajika,hivyo kusababisha haja ya kuanzishwa kwa kiwanda cha gundi. Matokeo ya shughuli hizi zote ni kuzalishwa kwa nafasi anuwaiza kazi kwa wakazi. Hili litakuwa na matokeo zaidi chanya,hususan kwa vijana. Badala ya kushiriki ulevi na burudani zinazowahatarisha, wataweza kumjitafutia riziki katika viwanda hivi.

Juu ya hayo,mfumo wa ugatuzi utayaweza maeneo husika kuongeza thamani,utoaji wa huduma za kijamii na kuitawala kulingana na mahitaji ya maeneo haya. Ni muhimu hata hivyo kuzingatia kwamba kila eneo laugatuzi lina upekee wake,navyo vipaumbele hutofautiana kulingana na maeneo. Kuna yale ambayo yatasisitiza usalama, mengine ujezi na uimirishaji wa miundomusingi kama vile barabara,vituo vya afya na hata taasizi za elimu. La muhimu ni wakazi wa maeneo husika kubainisha ni lipi litatekelezwa kwanza.

Kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Kufanikiwa kwa mfumo wa ugatuzi kutategemea juhudi za kila mkazi wa eneo husika. Ni muhimu kila mkazi kujiona kuwa mmiliki wa eneo zima la ugatuzi na kuwajibika katika kuliendeleza kwa hali na mali. Uwajibikaji huu unajumuisha uteuzi wa viongozi wenye muono mzuri na mabao utawawezesha kuyafikia malengo yao ya kimaendeleo. Hakika,mustakabali na uwepo wa eneo la ugatuzi utakuwa zao la mamuzi ya wanaeneo. Vilevile ufanisi wa maeneo ya ugatuzi utakuwa msingi wa ufanisi wa taifa kwa jumla.

(a). Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 85-90 (alama 8,1 mtiririko

Mtayarisho)

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

a) Kwa kutumia maneno 75-80, bainisha masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama 7,1 mtiririko) (Alama 8)

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

3. MATUMIZI YA LUGHA(Alama 40)

a) Andika sifa mbili mbili za sauti zifuatazo. (alama 2)

(i). /e/

……

……

……

(ii). /ch/

……

……

……

b). Unda maneno yenye muundo ufuatao wa sauti. (Alama 2)

KIKIKI……..

IKKI……

c). Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U-ZI (alama 2)

……

……..

d). Tunga sentensi moja moja kuonyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo. (alama.2)

i). Vifungo ……

ii). Kibainishi ……..

e). Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari (alama 2)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Mhadhara huo tata ulitolewa jana jioni.

……

f). Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa. (Alama 2)

Ndege hao wana manyoya mengi

……

……

g). Andika visawe vya maneno yafuatayo. (Alama 2)

i). Doa

……

ii). Omba

……

(h) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya riti na ridhi (Alama 2)

……

……

……

i). Bainisha silabi katika neno (Alama 1)

Wanyweshavyo

……

j). Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo (alama.2)

Mwenyewe alikipenda kwa dhati

……

……

……

k). Tumia kielezi cha kiasi badala ya kile kilichopigiwa mstari. (alama.2)

Msichana yule alizungumza kitausi.

……

……

l). Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi (alama.2)

safina alimwambia Asha kuwa angetembelea wazazi wao siku hiyo jioni.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

……

……

……

m). Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi (Alama 3)
Mvua kubwa inayonyesha itasababisha mafuriko.

……

……

……

n). Kanusha sentensi ifuatayo kwa wakati ujao hali ya kuendelea (Alama 2)
Walimu wanafunza

……

……

o). Andika upya setensi ifuatayo wa kuzingatia kauli iliyowekwa katika mabano (Alama 2)
yeye ni bahili itakuwa vigumu kumkopesha pesa. (kutendesheka)

……

……

(p) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya 'na' (alama 2)

……

……

……

……

q). Andika sentensi ifuatayo upya ukianzia yambwa tendewa (alama.2)
kirwa alimjengea mama huyo nyumba kwa mawe

……

……

r). Ainisha vishazi katika sentesi ifuatayo. (alama 2)
ingawa alitia bidi masomoni,alifeli mtihani.

……

……

s). Andika sentensi upya ukitumia vinyume vya maneno yaliyopigiwa mstari. (Alama 2)

Mama <u>alijitwika</u> kikapu mgongoni baada ya <u>kuinjika</u> chungu mekoni.

……

……

t). Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa.

i). umekuja (alama 2)

ii) Tumefurahi sana (unganisha sentensi hizi kwa kuanza na kuja…….)

……

……

……

ISIMU JAMII (Alama 10)

"Mwite mhandisi aukarabati mtambo huo"

a). Taja sajili inayorejelewa hapo juu. (Alama 2)

……

……

(b). Fafanua sifa zozote nne za sajili uliyoichagua (Alama 8)

……

……

KCSE PREDICTOR 1

102/3

KISWAHILI
Karatasi ya 3

FASIHI 102/3

SWALI LA KWANZA, SWALI LA LAZIMA

SEHEMU YA A: USHAIRI- (Alama 20)

Niokoa muokozi, uniondolee mashaka
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
Nimekitiri simanzi,ni katika kuudhika
Mja wako nasumbuka,nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka,nataka kwao afua
Nirehemu kwa haraka,nami nipate pumua
Naomba hisikitika,na mikono hiinua
Mtenda ndiwe moliwa,nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe moliwa,we ndiwe mola wa anga
Mazito kuyaondoa,pamoja na kuyatenga
Ukauepusha ukiwa,ya pingu zilonifunya
Nikundulia muwanga,nipate niyatakayo

Nikundulia muwanga,nipate toka kizani
Na huzuni n'ondolea,itoke kwangu moyoni
Mambo mema niegheshea,maovu nisitamani
Nitendea wa manani,nipate niyatakayo

Igeuze yangunia,dhaifu unipe mema

Nili katika dunia,kwa afia na uzima

Moliwa nitimizia,yatimize yawe mema

Nifurahike mtima,nipate niyatakayo.

Maswali

(a). Eleza bahari zozote mbili za shairi hili (alama 4)

(b). Eleza muundo wa shairi hili (Alama 4)

(c). Mshairi ametumia uhuru wake wa utunzi. Eleza mifano minne huku ukitoa mifano (alama 4)

(d). Andika ubeti wa pili katika lugha tutumbi (alama 4)

(e). Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili
(alama.2)

(f). Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi (alama 2)

(i). Nimedhihika

(ii). Nifurahike mtima

SEHEMU B: RIWAYA – ASSUMPTAMATEI - CHOZI LA HERI

2. Haki za watoto hazitiliwi maanane katika jamii nyingi za kiafrika. Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya chozi la heri (Alama 20)

au

3. "Kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika" (Alama 20)

a. Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)

b. Eleza namna msemaji alivyoukata mkono aliostahili kuuibusu. (alama 6)

(alama 14)

c. Eleza tamathali ya usemi unaojitokeza katika dondoo hili.
(alama.2)

d. Fafanua sifa nne za msemaji wa kauli hii (alama 8)

SEHEMU C: TATHILIA KIGOGO NA PAULINE KEA

4. ‘’Na hawa wafadhili wao nao lazima wavunje kambi zao. Sagamoyo twajiweza’’

a. Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b. Kwa kutolea mifano saba kwenye tamthilia eleza jinsi kauli hii ‘’Sagamoyo twajiweza’’ ni kinaya ?

(alama 14)

c. Mbali na kinaya tambua mbinu nyingine ya kisanaa katika dondoo hili (alama 2)

AU

5. Jadili mbinu wanazotumia wanasagamoyo kujikomboa kutoka utawala dhalimu wa Majoka

(Alama 20)

SEHEMU D: HADITHI FUPI - TUMBO LISILOSHIBA

6. “… Ningeondoka…..mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana”

b) Eleza muktadha wa maneno haya
(Alama 4)
c) Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili
(Alama 2)
d) ‘’Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja tisa
(Alama 9)

d). Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii
(alama.5)

AU

7. (a). Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya Masharti ya Kisasa (alama 13)

(b). Kwa kurejelea hadithi ya Shibe inatumaliza,eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitokeza

(alama 7)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8 (a) Miviga ni nini? (Alama 2)

(b) Fafanua sifa sita za miviga (Alama 6)

(c) Kwa nini jamii huthamini miviga (Alama 8)

(d). Onyesha udhaifu unaohusishwa na miviga (Alama 4)

\

KCSE PREDICTOR 2

102/1
KARATASI YA 1
INSHA
MUDA: 1 ¾

MASWALI

e) Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo.

Andika barua ya kuomba nafasi hii na uiambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi.

2. Jukumu la kuzuia msambao wa virusi vya korona ni la mtu binafsi. Jadili.

5. Andika insha itakyothibitisha ukweli wa methali
Mchelea mwana kulia, hulia mwenyewe.

6. Anza kwa.
Mwanangu, dunia imebadilika pakubwa lakini chunga mabadiliko hayo yasikuzuzue….

KCSE PREDICTOR 2

KARATASI 102/2
KISWAHILI

MUDA SAA 2 ½

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

1. UFAHAMU (Alama 15)

Huku ulimwengu unapoingia ya katika teknologia ya tarakilishi na sera ya utandaridhi, ukweli wa mambo ni kuwa akina mama wamezinduka. Suala la usawa wa kijinsia limeanza kushamiri kote duniani na ole wake mwanamume yeyote ambaye hajawa tayari kutembea na majira. Lakini hebu tuchunguze jambo hili kwa makini zaidi.

Usawa wa jinsia ni nini? Usawa wa kijinsia ni usawa wa binadamu wote; wawe wake au waume. Usawa huu unapaswa kudhihirika katika kugawa nafasi za kazi, utoaji wa elimu, nafasi za uongozi na Nyanja zinginezo zozote za maisha.

Ubaguzi wa aina yoyote ile hasa dhidi ya mwanamke ni jambo linalokabiliwa na vita vikali sana ulimwenguni kote.

Dahari na dahari, hasa katika jamii za kiafrika kumekuwa na imani isiyotingizika kuwa mwanamke ni kiumbe duni akilinganishwa na mwanaume. Kwa hivyo mwanamke amekuwa akifanyiwa kila aina ya dhuluma ikiwepo kupigwa, kutukanwa, kudharauliwa, kunyimwa haki zake, kunyimwa heshima na mambo kama hayo, lakini je, ni kweli kuwa mwanamke ni kiumbe duni asiyefaa kutendewa haki?

Tukichunguza jamii kwa makini tunaweza kuona mara moja kuwa hivyo ni imani potovu isiyo na mashiko yoyote. Ukimulika familia yoyote ile iliyopiga hatua kimaendeleo, uwezekano mkubwa ni kuwa mume na mke wa familia inayohusika wana ushirikiano mkubwa. Mume anamthamini mke wake na hadiriki kufanya maamuzi muhimu yanayoweza kuathiri maendeleo ya familia bila kumhusisha mke. Mume kama huyo huketi na mkewe, wakishauriana na kufikia uamuzi bora.

Tukitoka katika muktadha wa kifamilia na kumulika ulimwengu wa kazi iwe ni katika afisi za serikali au kwenye makampuni binafsi, ukwerli ni kwamba kiongozi yeyote yule aliyefaulu katika usimamizi wake mara nyingi huwa na mke nyumbani ambaye wanashauiriana kila uchao kuhusu kazi anayofanya hata kama mke hafanyi kazi mahali pale. Hisia na mawaidha anayotoa mke kwa mume wake ni tunu na huenda asiyapate kwingineko kokote hata katika vitabu vya kupigiwa mifano. Hii ni mojawapo ya sababu ambayo huwafanya viongozi wa nchi mbalimbali kupenda sana kuwatambulisha wake na familia zao waziwazi kwa vile wanajua kuwa jamii inathamini sana msingi wa jamii. Kiongozi ambaye hana mke au familia au yule ambaye hana mke wake hatambuliki, hutiwa mashaka na jamii hata kama ni kiongozi aliye na azma ya kushikilia kazi ngumu ya kuongoza umma.

Tukirudi nyuma kidogo na kupiga darubini mataifa ya mbali, tunaweza kuwaona wanawake mashuhuri walio uongozini ambao hadi waleo unapigiwa mfano. Wanawake mashuhuri waliotoa uongozini ambao hadi wa leo unapigiwa mfano. Wanawake hao walisimamia mojawapo ya mataifa yenye uwezo na ushawishi mkubwa Zaidi duniani. Ingawa wengi wao sasa wameng'atuka, uongozi wao bado unakumbukwa hata baada ya miaka mingi ya wao kuamua kupumzika ,mfano ni kama :Bi Bandranaike wa Sri lanka, Golda Meir wa Israel na wengine wengi katika mataifa kama Indonesia, Ufilipino, Bangladesh, Pakistani na kwingineko.

Katika kufikia tamati, tunapozungumza kuhusu jinsia, hatuna budi kugusia kitafsili masuala nyeti. Kwanza,imani ya kushikilia kikiki tamaduni zisizofaa, ni jambo linalofaa kuchunguzwa kwa makini. Kwa mfano, kuna badhi ya jamii ambazo humlazimu mke kurithiwa baada ya kifo cha mumewe. Vile vile baadhi ya jamiii za kiafrika zinanshikilia kuwa mwanamke hana haki ya kurithi. Kutokana na Imani hii, wanawake wengi huishi maisha ya taabu baada ya kutengana na waume zao kwa vile hawana haki ya kurithi chochote kutoka kwa wazazi wao hata kama wazazi hao wana mali nyingi kupindukia. Mali ya wazazi ni haki ya watoto wa kiume wala si watoto wa kike! Hili ni jambo la kusikitisha mno.

Isitoshe, wanawake hukumbukwa na kizingiti kingine wanapojaribu kumiliki mali ya waumezao baada ya waume hao kukata kamba .sababu ni kuwa,baada ya hao wenda zao kuwekwa kaburini, vita vya umiliki wa mali huanza mara moja na mwishowe yule mke maskini hujikuta hana hata mahali pa kulala sembuse mali waliyochuma na mali yake yote kunyakuliwa na aila ya mumewe . Jambo hili linaonyesha namna tulivyoachwa nyuma na uhalisia wa mambo. Ni lazima jamii izuinduke na itoke kwenye kiza hiki chenye maki nzito.

MASWALI

a. Ina maana gani kusema kuwa wanaume hawana budi "kutembea na majira"

_____

_____

_____(alama 2)

b. Kabla ya uzinduzi huu kuhusu usawa wa jinsia, wanawake wamekuwa wakitendewa dhuluma za kila aina. Taja tatu.

_____

_____

_____

_____ (alama 3)

c. Je, ni kwa nini viongozi wengi hupenda kujitambulisha na familia zao?

_____

_____

_____(alama 2)

d. Je, unaamini kuwa hisi na mawaidha anayatoa mke wa mume wake ni tunu na huenda yasipatikane kwingineko? Fafanua

_____

_____

_____(alama 2)

e. Je, licha ya kunyimwa haki yake ya kujiamulia, ni matatizi yapi mengine yanayoweza kumkumba mke anayelazimishwa kurithiwa?

_____

_____

_____ (alama 3)

f. Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika hali muktadha. (alama 3)

Kushamiri

_____

_____

Hulka

_____

_____

Azma

2. MUHTASARI

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo.

Idadi kubwa ya wanafunzi huingiwa na wasiwasi wakaribiapo kufanya mtihani kwa sababu mbalimbali, kubwa likiwa ni hofu kwa jinsi ambavyo watafanya katika mtihani huo. Asilani mambo hayafai kuwa hivyo. Wataalamu wa masuala ya saikolojia na wale wa elimu wanashauri kuwa mtahiniwa anafaaa kupata muda mwingi wa mapumziko wakati anapokaribia kufanya mtihani ili aweze kituliza akili asije akapatwa na mzongo wa akili.

Moja katika mashauri ni kuwa mtahiniwa anafaa kupata usingizi wa kutosha wakati akijiandaa na pia wakati akifanya mtihani. Hii ni kwa sababu mtihani wa mwisho si tofauti na mitihani mingine ambayo mtahiniwa amekuwa akifanya, pamoja na kuwa ni maswali ya jumla tu kutoka viwango vyote vya masomo. Hivyo basi, mtihani unapokaribia, mtahiniwa anafaa kudurusu na kufanya majaribio mbalimbali ya mtihani pamoja na kujikumbusha yale aliyofunzwa na mwalimu wake. Wale asimdunishe au kumdharau mwalimu hata kama stadi zake za kufundisha kazikumsisimua – alikupa kito cha thamani kitakachokufaa kama silaha wakati wa mtihani.

Mtihani unapokaribia, mtahiniwa anafaa kuwa amekwisha kutambua udhaifu wake na kutia bidii kuudhibiti kupitia udurusu, mijadala na mashauriano. Kumbuka kuwa bidii haiui ila hulipa. Hivyo basi, kila unaposhirikisha bidii na ujasiri wa wako na kuimarisha uelewe wako wa somo, na hatimaye ukaboresha matokeo katika somo hilo. Vilevile, kujadili au kufafanua mada unayoielewa vyema kwa m wenzio aiyeielewa kutakuwezesha kuielewa hata Zaidi na hivyo kuimarisha uwezo wako wa kuzoa alama nyingi katika mtihani endapo swali litatoka katika mada hiyo.

Pamoja na hayo, mtahiniwa anafaa kujihadhari na majuto ya kufanya kile ambacho hakupaswa kufanya. Anaweza kuhakikisha hili kwa kuyapitia maswali kwa makini Zaidi, na kuyatafakaria, kuyapangia na kuaandikia majibu sawasawa kasha kuyasoma tena majibu yake ili kuwa na uhakika kwamba hajapotoka.

Ikiwezekana (kwa sababu ya tofauti za kimapato na uwezo wa wazazi au walezi) mtahhiniwa anafaa kula visuri kabla kuenda kufanya mtihani. Vilevile, anapaswa kufika katika chumba cha

mtihani kwa wakati unaofaa – mapema kabla ya muda wa kuanza kwa mtihani – na ahakikishe amebeba kila kifaa atakachokihitaji katika mtihani huo.

Ikiwa utashindwa kujibu swali Fulani, usipotezee muda mwingi. Baadala yake, enelea na swali linalofuatia kasha ulirejelee swali lile lililokutatiza baadaye ukishamaliza maswali yale mengine. Usipoteze muda kutafuta jibu ambalo huna kwa wakati huo. Juu ya yote, usidhubutu kuifanya hila katika mtihani kwa kuwa kitendo kama hicho kitasababisha matokeo yako kufutiliwa mbali, nayo bidii yako ya miaka mine itakuwa imeishia gizani, ukasalia kujuta.

Maswali.

f) Tumia maneno 60 kueleza ujumbe ulio katika aya mbili za mwanzo. (alama 6)
Nakala chafu

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

Jibu

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

g) Mwandishi anatoa ushauri gani kwa mtahiniwa katika aya ya tatu hadi ya mwisho? Eleza kwa maneno 100 (alama 9)

Nakala chafu

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

Jibu

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
___

SEHEMU C - MATUMIZI YA LUGHA.

a) Eleza ufauti ya kimsingi iliyopo kati ya irabu na konsonanti.

_____
_____
_____ (ala2)

b) Taja sifa tatu bainifu za irabu /O/

_____
_____
_____
_____
_____(ala 3)

c) Andika maneno yenye muundo ufuatao

i) KKKIKI

_____

_____

ii) KKIKI

_____

_____(ala2)

d) Andika tungo ya neno moja yenye viambishi vifuatavyo.

7. Nafsi

_____

8. Njeo

_____

9. Kirejeshi

_____

10. Shamirisho

_____

11. Mzizi

_____

12. Kauli ya kufanyiza

_____

13. Kiishio

_____ (ala3)

e) Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeana. (ala2)

i) –la

_____

ii) – nywa

f) Andika sentensi ifuayo kulingana na maagizo. (ala2)

Maagizo

Mhalifu <u>alisamehewa</u> kwa sababu <u>alinyenyekea .</u>

Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino.

_____

_____

g) Andika kwa wingi

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Kelele ya amchaye Mungu ni baraka.

_____

_____(ala1)

h) Tambua aina ya vishazi katika sentensi hii
Utazawadiwa ukicheza vizuri.

_____

_____ (ala2)

i) Tofautisha matumizi yapo katika sentensi hizi. (ala2)
   a) Alipomwona alimhoji.
   b) Amwonapo humhoji

_____

_____

j) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari. (ala2)
Ubaguzi <u>wa kijinsia</u> umekashifiwa mno na <u>viongozi wenye msimamo thabiti mno</u>.

_____

_____

_____

k) Unda nomino kutokana na vitenzi (ala2)
   1. Jaribu

_____

   2. Chuma

_____

l) Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi
Wageni <u>na</u> wenyeji walikimbili<u>ana</u>

_____

_____ (ala 2)

m) Andika katika msemo wa taarifa. (ala3)
"Nitakuarifu nikimwona" Maria alisema

_____

_____

n) Eleza maana mbili za sentensi (ala2)
Tuliitwa na Juma

o) Tumia "0" rejeshi katika sentensi ifuatayo
Mtu ambaye hutupa tope hujichafua mwenyewe.

_____

_____(ala 2)

p) Tumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika tena sentensi ifuatayo.
Ukuta umemwuumiza mvulana alipokuwa akiuparaga.

_____
_____
_____ (ala3)

q) Changanua sentensi kwa njia ya jedwali.
Ouma alianguka mtihani ila Kamau alifuzu vizuri.

_____
_____
_____
_____
_____ (ala4)

ISIMUJAMII

Mtu 1: Wewe njoo hapa (kwa sauti kubwa) fanya upesi.
Mtu II : (anakimbia mbio) Naja Sir
Mtu I : (anamtazama) unajifanya mwelevu?
Mu II : Hapana Sir……eh…..afande
Mtu I : Jina
Mtu II : Samwel Kioko
Mtu I : (Huku akiandika) Lete kitambulisho
Mtu II : Sina hapa sir
Mtu I : Huna kitambulisho? Utafanyiwa booking vipi?
Mtu II : Naomba
Mtu I : Naomba ! naomba! Unaomba nini? Wazururaji kama nyinyi tunawajua. Mnajifanya hamjui kuna curfew. Mnajiponza, "zerikali saidia". Usiniharibie muda wangu (akiashiria) ingia ndani! Utakuwa mgeni wetu leo. Tutakukarimu chakula cha chumba.(anamsukuma ndani)

(i) Bainisha sajili ya makala haya.

_____
_____
_____(ala2)

(ii) Eleza sifa nne za sajili kwa kurejelea makala haya.(ala 8)

_____
_____
_____
_____
_____

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 2

KARATASI YA TATU – 102/3

FASIHI

MUDA: 2 ½

1. FASIHI SIMULIZI: SWALI LA LAZIMA

a) *Miviga ni nini?* Al.2

_____

_____

b) *Eleza sifa tano za miviga.* Al.5

_____

_____

_____

_____

_____

_____

c) *Fafanua hasara tatu za miviga.* Al.3

_____

_____

_____

_____

d) Eleza changamoto tano ambazo mtafiti hukabiliana nazo anapokusanya data ya fasihi simulizi. *Al.5*

_____

_____

_____

_____

_____

_____

e) *Eleza majukumu ya wimbo katika hadithi.* Al.5

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

TAMTHLIA: KIGOGO

2. **Tulipoanza safari hii matangazo yalikuwa bayana, dhahiri shahiri babu!**
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. ***Al.4***

   _____

   _____

   _____

   _____

   _____

   b) Tambua mbinu za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki. ***Al.4***

   _____

   _____

   _____

   _____

   c) Eleza matatizo yanayokumba safari inayorejelewa. ***Al.12***

   _____

   _____

   _____

   _____

3. **Tamthlia ya kigogo inazungumza kuhusu hali halisi katika mataifa mengi ya kiafrika. Jadili**. **Al.20**

4. **RIWAYA: CHOZI LA HERI**

   "***Alikumbuka jinsi rafiki yake……..alivyofishwa kwa njia hii. Akili yake ilimtambia kisa chenyewe kana kwamba inataka kumwonya (uk.120)***

   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. Al.4

   _____

   _____

   _____

   _____

   _____

   b) Bainisha tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. Al.4

c) Tathmini nafasi ya anayelengwa na kauli hii katika kuijenga riwaya hii. Al.12

5. a) Fafanua namna mbinu ya majazi ilivyotumiwa katika riwaya. Al.10
   b) Jadili maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii ukirejelea riwaya ya Chozi la Heri. Al.10

6. <u>HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA</u>

a) Eleza ufaafu wa anwani mapenzi ya kifuaurongo kwa kurejelea mhusika Penina. Al.10

b) Eleza nafasi ya elimu katika maisha ya wanajamii ukirejelea hadithi: Mtihani wa maisha. Al.10

7. a) **<u>Mame Bakari</u>**

*"**Una nini? Umeshtuka mwanangu! Unaogopa? Uaogopa nini?***

b) Weka dondoo hili katika muktadha wake. *Al.4*

c) Eleza sifa za mrejelewa. ***Al.6***

d) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo. ***Al.2***

e) Eleza umuhimu wa msemaji. ***Al.4***

_____

_____

f) Tambua maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki. *Al.1*

_____

_____

g) Fafanua maudhui katika swali la (e) kwa kurejelea hadithi nzima. *Al.3*

8. USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali

Alikwamba wako mama, kajifanya hupliiki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo!Hutaki
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo h adaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Manchangu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
Na tena ukajiona, kwamba we mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mwenyewe!

MASWALI

a) Eleza dhamira ya shairi hili. *Al.2*

_____

_____

b) Tambua njia mbili anazotumia mtunzi wa shairi hili kusisitiza ujumbe wake.Al.2

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

_____

_____

c) Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi. ***Al.4***

_____

_____

_____

_____

d) Andika ubeti wa tatu katika lugha tutumbi. ***Al.4***

_____

_____

_____

_____

e) Bainisha toni ya shairi hili. ***Al.2***

_____

_____

f) *Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili.* Al.4

---

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. ***Al.2***

i) Mstahiki

_____

_____

ii) Hupuliki

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 3

102/1
INSHA
KISWAHILI
MUDA: SAA $1^{3}/_{4}$

1. Andika **tahariri** kuhusu sababu za kudorora kwa usalama katika gatuzi lako.

2. Fafanua hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa nchini kukabiliana na umaskini nchini

3. Andika insha inayooana na methali ***mchuma janga hula na wa kwao.***

4. Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo.

...niliyagugumia maji hayo kwa pupa na kung'amua kuwa maji ni uhai.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

KCSE PREDICTOR 3

102/2

KISWAHILI: LUGHA

MUDA: SAA 2½

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Ilikuwa jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa kusikiliza taarifa ya habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe kiinuamgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi laki mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki.

Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, waziri wa kilimo alitangaza bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia la kilo tisini. Nami nilikuwa naanza kuumakinikia mradi huu.

Baada ya taarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichukua mara moja. Usingizini niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kulima nilitenga ekari kumi za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wakati wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nililipa shilingi elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejo. Kwanza, nililipa shilingi 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunua magunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilingi 3,300 kila gunia. Mwezi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazo bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilingi 1,000 kila ekari. Mvua ilinyesha vizuri na baada ya siku saba, mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya

kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mbegu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua na kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilia kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo 'amonia'. Gharama yake ikawa shilingi 1,300 kila gunia. Hivyo nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano.

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa mashina. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapitanjia waliajabia mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siku wanaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanisi wangu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata na kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa 'Usikate majani, mnyama hajauawa.'

Bila taarifa wala tahadhari, mvua ilitoweka. Hayakupita majuma mawili mahindi yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahindi, shamba likageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makisio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi ufanyavyo moshi. Lakini 'Muumba ndiye Muumbua.' Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha. Muda si muda mahindi yalianza kunawiri. Kumbe tuko lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafu huku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba niliona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli.

Muda si mrefu mahindi yalirudia hali yake tena, kisha yakakomaa. Harakati za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli hii ikawa shilingi 5,000. Kuvuns, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. Habari motomoto siku hiyo ilikuwa. 'MAHINDI GUNIA 900/=.' Niligutuka usingizini.

Maswali

(a) Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari. (alama 1)

_____

(b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika? (alama 2)

_____

_____

(c) Taja matatizo matatu yaliyotishia mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi (alama 3)

_____

_____

_____

(d) Eleza maana za methali zifuatazo kwa mujibu wa taarifa

(i) Usikate majani, mnyama hajauawa (alama 1)

_____

(ii) Muumba ndiye muumbua (alama 1)

_____

(e) Eleza mambo mawili yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia. (alama 4)

_____

_____

_____

_____

(f) Kwa nini msimulizi alisema maumbile ni kitu cha ajabu? (alama 1)

_____

(g) Eleza maana za;

i. Kinuamgongo (alama 1)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

ii. Manyakanga wa kilimo (alama 1)

2. UFUPISHO(ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ufupishe kwa mujibu wa maswali uliyopewa
Utafiti umebaini kuwa pana uwiano baina ya lugha inayotumiwa kwa lugha rasmi na kiwango cha umaskini katika nchi, na pia kiwango cha ustawi. Kwa mfano, nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikitumia lugha za wakoloni waliozitawala kama lugha rasmi. Nchi hizi zimekuwa zikitumia lugha hizo katika shughuli rasmi, kutoa mafunzo na kupitishia sera muhimu zinazoathiri maisha ya wananchi wote. Kile wasichozingatia ni kuwa, raia wao wengi hawazielewi.

Idadi kubwa ya raia barani Afrika ni wakulima au wasakatonge katika sekta za juakali, uchukuzi na biashara ndogondogo ambao hawana umilisi wa lugha hizo za kigeni. Watu hawa aghalabu huendesha shughuli zao za kila siku kwa kutumia lugha zao za asili, au kama hapa Afrika MAshariki, hutumia Kiswahili ambacho aghalabu hawazingatii usanifu wake. Je, kwa nini tusiokoe na kuauni idadi hii kubwa ya watu ili kuimarisha hali zao kiuchumi, kijamii na ambazo hawazielewi; lugha zinazotumiwa na kufahamika na wachache?

Manufaa ya kutumia lugha inayoeleweka ma kufahamika na wengi kama lugha rasmi ni lukuki yakilinganishwa na maumizi ya lugha za kigeni kama kiingereza, kifaransa, kijerumani au kimandarin. Kwanza, matumizi yake huwawezesha watumiaji kujieleza wakaeleweka vizuri kwa kuwa mkondo wa fikra unatumia lugha wanayoijua, na hivyo wana nafasi ya kuwa wabunifu. Kwa mfano, matumizi ya lugha asili katika utoaji elimu yatahakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki kikamilifu katika shughuli zote za kielimu. Hawatakuwa wanafunzi wanaongojea kuelezwa kila kitu bali watajisakuria ili kujizidishia maarifa.
Matumizi ya Kiswahili, lugha inayoeleweka na idadi kubwa ya watu, huhakikisha kuwa ujuzi na maarifa yanayopitishwa si himaya ya kundi dogo tu lililoelimika bali hata wale wasiobahatika kuzielewa lugha hizo za kigeni. Hii ni kwa sababu anayesema kwa lugha ya kigeni husema na ubongo, naye asemaye kwa lugha asili husema na moyo, hivyo basi akaeleweka zaidi katika yale ayasemayo. Aidha, matumizi haya hutoa nafasi sawa kwa wengi na kuepusha

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

utegemezi wa wakalimani ambao aghalabu hawaeleweki kutokana na kasi ya mazungumzo, au wakatoa fasiri isiyo sahihi. kila mmoja ataweza kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa kutokana na uwezo wa kufasiri sera za serikali na kutoa uamuzi wao wenyewe ikilinganishwa na wakati ambapo sera hizi zinawasilishwa kupitia lugha za kigeni.

Fauka ya haya,matumizi ya lugha inayoeleweka na wengi huwawezesha watu kushiriki na kuchangia katika uimarishaji wa demokrasia kutoka vijijini, hadi kitaifa. Hata hivyo, itashangaza kumwona mzungu akizungumza na wanajamii kwa Kiswahili, naye mwakilishi wa jamii hiyo akiwazungumzia kwa kiingereza. Hii ni njia mmoja ya kuwatenga raia wasioelewa lugha hiyo ya kigeni. Matumizi ya lugha kama hii huhujumu mtagusano baina ya watu. Kwa hivyo, hakisalii tu kuwa lugha rasmi katika katiba bali katika uhalisia.

Maswali

(a) Fupisha aya ya kwanza kwa kutumia maneno 35-40 (alama 5)

Nakala chafu

_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____
_____

Nakala safi

_____
_____
_____
_____
_____
_____

(b) Kwa maneno kati ya 100-110, eleza manufaa ya kutumia lugha inayoeleweka na watu wengi kama lugha rasmi katika nchi. (alama 10)

Nakala chafu

Nakala safi

3. <u>SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)</u>

(a) Taja vipasuo viwili vya kaakaa laini. (alama 2)

(b) Andika neno lenye sauti mwambatano. (alama 1)

(c) Weka shadda katika neno lifuatalo ili itoe maana mbili tofauti. (alama 2)
ala

_____

_____

(d) Tumia kiimbo katika sentensi mbili tofauti ili kudhihirisha. (alama 2)

i. Ombi/rai

_____

ii. Amri/kuamuru

_____

(e) Tambulisha vipashio vinne vya sarufi ya Kiswahili. (alama 2)

_____

_____

(f) Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru nafsi ya tatu wingi. (alama 2)

_____

_____

(g) Tumia kivumishi cha pekee katika sentensi kuonyesha umilikaji. (alama 1)

_____

(h) Tumia vihusishi kuonyesha uhusiano wa wakati na kiwango. (alama 2)

_____

_____

(i) Weka maneno haya katika ngeli zake. (alama 2)

i. Miwani

_____

ii. Wema

_____

(j) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. (alama 3)

Hakuwakaribisha

_____

_____

_____

(k) Bainisha tofauti kati ya mzizi huru na mzizi funge kwa kutoa mifano. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(l) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika senensi ifuatayo. (alama 2)
Utakapomkabidhi barua hii, nipashe habari

_____

_____

(m) Tambua aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Ilitumwa kumlimia nyanya shamba

_____

_____

_____

(n) Yakinisha sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (alama 2)
Hakuwasaidia wala hakuwakaribisha kwake.

_____

_____

(o) Tambua kirai kihusishi katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Jino la Tamma linauma mara kwa mara.

_____

(p) Tunga sentensi ukitumia neno zawadi kama kitenzi (alama 2)

_____

_____

(q) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)
“Nitamwalika mtondogoo.” Fatuma akasema.

(r) Changanua sentensi hii kwa kutumia matawi. (alama 4)
Darasa lilojengwa limefunguliwa leo alasiri.

(s) Kanusha (alama 1)
Sisi ndisi wanafunzi

(t) Tunga sentensi moja ukitumia kiambishi –po- kudhihirisha mahali dhahiri. (alama 1)

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza maana ya lugha ya taifa. (alama 2)

(b) Eleza sababu tatu zinazofanya watu kubadili na kuchanganya ndimi. (alama 3)

(c) Eleza hatua tano ambazo zimesaidia kukuza lugha ya Kiswahili baada ya uhuru nchini Kenya. (alama 5)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

KCSE PREDICTOR 3

102/3
KISWAHILI
Karatasiya3
FASIHI
MUDA: SAA 2 ½

SEHEMU A: TAMTHILIA

P. Kea: *Kigogo*

1. **Lazima**

Soma kifungu ufuatao kisha ujibu maswali.

(a) Utaiondoa karaha,
Usiwe kama juha,
Kujipa bure usheha,
Kutembea kwa madaha,
Eti waenda kwa staha,
Ndani kwa ndani kuhaha,
Domo mbele kama mbweha.
Dume acha mzaha,
Shika lako silaha,
Kujipa mwenyewe raha,
Iwe yako shabaha.

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Taja mtindo huu wa uandishi. (alama 1)

(iii) Bainisha tamathali **moja** ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 1)

(iv) Fafanua majukumu ya nafsineni katika tamthilia *Kigogo.* (alama 4)

(b) Kwa kurejelea wahusika mbalimbali katika tamthilia Kigogo. Eleza jinsi mwandishi alivyofanikiwa kutumia nyimbo kuendeleza maudhui, (alama 10)

SEHEMU B: RIWAYA (CHOZI LA HERI)

Jibu swali la 2 au 3

2. “Kumbe hata mja akafanikiwa vipi kielimu na kitaaluma, maisha yake huwa ombwe bila mwana, awe wa kuzaa au wa kulea?”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Taja tamathali moja iliotumika katika dondoo (alama 1)

(c) Onyesha ukweli wa kauli hii ukirejelea wahusika wowote **watano** riwayani (alama 5)

(d) Fafanua umuhimu wa elimu katika jamii ukirejelea riwaya nzima. (alama 10)

3. “Una bahati kupata mfadhili, mimi mzazi wangu wa pekee ni mama ambaye ni muuza samaki na baada ya ule mzozo… biashara imepigwa na mawimbi makali.”

(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)

(b) Jadili jinsi mwandishi alivyoshughulikia maudhui ya ufadhili. (alama 6)

(c) Ukirejelea hadithi zozote tano riwayani, onyesha jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya hadithi ndani ya hadithi kujenga maudhui.(alama 10)

SEHEMU C: USHAIRI

Jibu swali 4 au 5

4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofauta.

SIONDOKI

1.

Eti

Niondoke!

Mimi niondoke hapa

Niondoke hapa kwangu!

Nimesaki; licha ya risasi

Vitisho na mauaji, siondoki.

2.

Mimi

Siondoki

Niondoke hapa kwangu!

Kwa mateke hata na mikuki

Marungu na bunduki, siondoki.

3.

Hapa

Siondoki

Mimi nipahame!

Niondoke hapa kwangu!

Fujo na ghasia zikizuka

Na kani ya waporaji, siondoki.

4.

Haki

Siondoki

Kwangu siondoki

Niondoke hapa kwangu!

Nawaje; waje wanaokuja

Mabepari wadhalimu, siondoki.

5.

Kamwe

Siondoki

Ng'oo hapa kwangu!

Katizame chini mti ule!

Walizikwa babu zangu, siondoki.

6.

Sendi

Nende wapi?

Si'hapa kitovu changu!

Niondoke hapa kwangu

Wangawa na vijikaratasi

Si kwamba hapa si kwangu, siondoki.

7.

Katu

Siondoki

Sihitaji karatasi

Niondoke hapa kwangu

Yangu mimi ni ardhi hii

Wala si makaratasi, siondoki.

MASWALI

(a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)

(b) Fafanua sifa mbili za nafsineni (alama 2)

(c) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

(d) Eleza umuhimu wa kihisishi katika shairi (alama 2)

(e) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia usambamba katika shairi (alama 2)

(f) Ukirejelea shairi, eleza namna mtunzi alivyotumia idhini zifuatazo (alama 3)

i) Inkisari

ii) Kufinyanga lugha

iii) Udondoshaji wa neno

(g) Taja mbinu tatu za lugha katika shairi (alama 3)

(h) Toa mfano mmoja mmoja wa mishororo ifuatayo (alama 2)

i) mshororo mshata

ii) mshororo kifu

5. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.

SHAIRI LA A

Falaula ngalijua, singalikuwa kijana,

Kwa sababu sikujua, kajipata mvulala,

Mengi mambo nikajua, nikashinda wasichana,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Mwili wangu kabadilli, toto hadi utu uzima,

Sauti yangu kabadili, nikajiola mzima,

Kakiuka maadili, dunia nikaizima,

Kweli ujana moshi, ukienda haurudi.

Masikiongu katonga, herini nikavalia,

Nywele yangu nikasonga, na mikufu kuvalia,

Video pia runinga, tazama bila tulia,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Malaika kapata, moyo wangu kapambika,

Jina lake kaloreta, mie wangu malaika,

Penzi langu kalipata,mambo mengi katendeka,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Moyongu kausumbua, nilipomtia mboni,

Penzi lanisumbua, aingiapo moyoni,

Sautiye kazindua, yatoa nyoka pangoni,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Penzi lake kalionja, kwangu likawa asali,

Nikawa kionjaonja, kuliwasha kawa kali,

Vitabungu nikakunja, navyo kavitupa mbali,

Kweli ujana ni moshi , ukienda haurudi.

Mzigo kabebesha, ukamwachisha skuli,

Mashakani kaniingisha, nikawa sasa silali,

Kulisaka suluhisho, likawa sasa ghali,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

SHAIRI LA B

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Mhariri nipe fursa, nifichue jambo hili,

Nipige wengi msasa, nakusihi tafadhali,

Ukweli wajue sasa, wamakinike ki hali,

Samaki pale barini,kweli huwa si mmoja.

Nawajuza mahawara, pale walipo hakika,

Si ya neni kihasira, ukweli nautamka,

Wayaepuke madhara, wazidi kumakinika

Samaki pale barini, kweli huwa si mmoja.

Dunia imegeuka, waja leo wana shani,

Wazidi kuhangaika, watatizika moyoni,

Utesi umeshazuka, mashambani na mijini,

Samaki pale barini, kweli huwa si mmoja.

Mahaba yakigeuka, hakika huwa ni dhiki,

Ugomvi uje kuzuka, uharibu urafiki,

Wakosane washirika, wapigane kila mwezi,

Samaki pale barini, kweli si mmoja.

Lakini sasa tengeni, vigogo niwasaili,

Iwapo ni hayawani,mpungufu kiakili,

Unisamehe sabini, kwa kosa moja kwa kweli,

Samaki pale barini kweli huwa si mmoja.

Hakika huwa si vyema, kibaya kukimiliki,

Mchongaji nayasema, natangaza uhakika,

Mtu mate huyatema, iwapo hayamezeki,

Samaki pale barini, huwa si mmoja.

Nafumbua fumbo wazi, mnielewe vizuri,

Nafasili ya mapenzi, yalokumbwa nazo zari,

Yalofitinika wazi, hapo ndipo nashauri,

Samaki pale barini, huwa si mmoja

Maswali

a) Jadili maudhui katika shairi A na shairi B (Alama 6)

b) Eleza muundo wa shairi la A (Alama 4)

c) Toa mifano ya uhuru wa utunzi uliotumiwa katika shairi la B. (Alama 2)

d) Andika ubeti wa nne wa shairi la A katika lugha nathari. (Alama 4)

e) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika mashairi haya. (Alama 4)

i) Nikajiola

ii) Mzigo kambebesha

iii)Shani

iv) Zari

SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

6. *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

(a) **A**: Kumbe mambo yenyewe rahisi hivi?

B: Rahisi, lakini usije ukabakwa tena

A: Hapana, safari hii itakuwa zamu yako. *(Alimrudishia ... huku akichekacheka)*

C: Hapajaharibika mambo mama'ngu. Kwani la ajabu lipi? Sasa miye namsubiri Bakari mpya tu, hichi kikongwe nikipe talaka.*(Akitabasamu)*

D: Haachwi mtu hapa. Tutabanana humo humo. Yeye atakuwa mke mdogo na mimi mkubwa.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 1)

(ii) Toa sababu **mbili** kuthibitisha jibu lako la (i) hapo juu. (alama 2)

(iii) Eleza manufaa saba ambayo jamii hunufaika nayo kwa kushiriki katika kipera hiki. (alama 7)

(b) *Soma kifungu ufuatao kisha ujibu maswali*.

Siwezi kuhututubu. Mimi sikuwafundisha ubaguzi. Kwa nini mnabaguana? Kwa nini hamukuwapa watu wa matabaka yote nafasi ya kuzungumza? Kwa nini? Kwa nini mnafanya hali hii ya kuwa kuna watu na nusu watu? Nataka wazungumze wale ambao hawata sifu tu.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 2)

(ii) Eleza mitindo mitatu katika kifungu hiki. (alama 3)

(iii) Eleza majukumu matano ya kipera hiki katika jamii. (alama 5)

SEHEMU E: HADITHI FUPI

Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine

"Tulipokutana Tena" **(Alifa Chokocho)**

5 (a) Halikuwa jambo la kawaida maana maji yalikuwa hayapatikani karibu pale kijijini petu. Sharti mtu aende masafa marefu kuyatafuta. Na sabuni? Sabuni ilikuwa kitu cha anasa kwa familia yetu. Wazazi wangu hakuwa na uwezo wa kununua Sabuni. Labda mara moja moja siku za sikukuu.

(i) Eleza muktatha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Eleza majukumu mawili ya **takriri** katika dondoo hili. (alama2)

(iii) Kwa kurejelea hadithi*Tulipokutana Tena* jadili jinsi haki za watoto zinavyokiukwa.(alama 6)

(b) Jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa ukirejelea hadithi zifuatazo: (alama 10)

(i) Masharti ya Kisasa

(ii) Ndoto ya Masha

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 4

102/1

KISWAHILI

Karatasi 1

Muda: Saa 1¾

INSHA 102/1

a) Lazima :

Wewe ni mwenyekiti wa jopo lililoteuliwa kuchunguza chanzo cha utovu wa usalama kijijini Sokoto. Andika ripoti maalum /rasmi kuhusu jambo hili.

b) Magonjwa mengi yanasababishwa na mitindo ya kisasa ya maisha.
Jadili.

c) Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mchagua nazi hupata koroma.

d) Andika insha itakayoanza kwa maneno haya:
Milipuko mikubwa ilisikika pu! Pu! Puu! Kisha niliwaona watu wakikimbia kuelekea pande zote…

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

KCSE PREDICTOR 4

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

MUDA: SAA 2 ½

1. UFAHAMU: (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. Inakera zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi,

aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea had kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo nakuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale hushia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine hushia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali 'mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**

_____

_____

b) Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu. **(alama 2)**

_____

_____

_____

_____

c) Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 2)**

_____

_____

_____

_____

d) Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa. **(alama 4)**

_____

_____

_____

_____

_____

e) Eleza haki mbili za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 4)**

_____

_____

_____

_____

_____

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu. **(alama 2)**

i) Inakera

_____

_____

ii) Majukumu

_____

_____

2. UFUPISHO: (Alama 15)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundishia. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkemu kwa mtu wa kila rika. Halikadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanaowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka

hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

a) Fupisha aya tatu za kwanza za (maneno 70 – 75) (alama 7, 2 za utiririko)

Matayarisho

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Jibu

_____

_____

_____

_____

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

b) Eleza udhaifu wa runinga na video. (maneno 50 – 51) (alama 5, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA: (alama 40)

a) Taja aina mbili kuu za ala za kutamkia sauti **(alama 2)**

b) Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo **(alama 2)**

Kimadende_____

Kipasuo kwamizo_____

c) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili **(alama 2)**

_____

_____

_____

_____

d) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo **(alama 3)**

Tulimpikia_____

e) Ainisha vitenzi katika sentensi: Kitabu anachotaka kusoma ki mezani **(alama 3)**

_____

_____

_____

_____

_____

_____

f) Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi kiteuzi **(alama 2)**

_____

_____

_____

g) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama 2)**

a) Uzi_____

b) Muda_____

h) Tumia ‘o’ rejeshi ya kati katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Watu ambao walifika jana ni wale ambao walitoka mbali

_____

i) Onyesha shamirisho kipozi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Mwindaji haramu alimuua ndovu kwa bunduki

_____

_____

_____

j) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 3)**

Kilipikwa jana jioni

_____

_____

_____

_____

k) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama 2)**

Msingesoma kwa bidii, msingepita

_____

_____

_____

_____

l) Tunga sentensi moja kudhihirisha dhamira/jukumu hili **(alama 2)**

Rai/ombi

_____

_____

_____

_____

m) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mtoto ambaye alianguka jana ana maumivu mengi

_____

_____

_____

_____

n) Onyesha matumizi yoyote mawili ya kiwakifishi: koma/kituo **(alama 2)**

_____

_____

o) Tumia neno 'Nairobi' kama **(alama 2)**

a) Nomino

b) Kielezi

p) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya kuku na gugu **(alama 2)**

q) Onyesha matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi **(alama 2)**

Mwongeleaji stadi anajishaua sana.

r) Andika katika usemi wa taarifa **(alama 2)**

"Wageni wangu watafika saa ngapi? Mama aliuliza

_____

_____

_____

s) Unda nomino kutokana na kitenzi **(alama 1)**

Safari

_____

_____

_____

4. ISIMUJAMII: **(alama 10)**

Nipe chai, andazi mbili na egg moja…….

a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya **(alama 2)**

_____

_____

_____

b) Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo **(alama 8)**

_____

_____

_____

_____

_____

_____

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 4

102/3(FASIHI)

KISWAHILI

KARATASI YA 3

MUDA: SAA 2

SEHEMU YA A: RIWAYA YA : CHOZI LA KHERI(ASSUMPTA .K. Matei)

1.Swali la Lazima

A. ``Kumbe hata wewe shemeji.....upo?''
``ndio tu hapa na wengi''
i.Eleza muktadha wa dondoo hili.
alama 4
ii.`Wengi ' wanaorejelewa katika dondoo hili walikumbwa na matatizo yapi?
alama 8

B.``Kule kulazimika kupapasa kwenye giza kutafuta.....''
Mrejelewa katika kauli hii anayafichua maovu yapi katika jamii?
alama 8

SEHEMU YA B. TAMTHILIA KIGOGO (Pauline kea)

2.``Huu moyo wangu wa huruma nao.....''
i.Eleza muktadha wa dondoo hili.
alama4
ii.Fafanua sifa za msemaji.
alama 4
iii.Onyesha kinyume kinachojitokeza katika dondoo hili.
alama 12

3.Vijana katika tamthilia ya kigogo wamesawiriwa kwa jicho hasi. Fafanua
alama 20

SEHEMU YA C. HADITHI FUPI

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE (WAHARIRI: A CHOKOCHO NA D. KAYANDA)

4. `.....Lakini shogake..... shogake..... shogake dada nikamwona ana ndevu'.

a. Eleza muktadha wa dondoo hili.
alama 4
b. Bainisha sifa tatu za `shoga ' anayezungumziwa katika dondoo hili.
alama 6
c.Jadili umuhimu wa `dada' anayerejelewa katika kuendeleza dhamira ya hadithi.
alama 10

5.``Wahusika katika hadithi shibe inatumaliza wanatumia uhuru wao vibaya.''Onyesha ukweli wa kauli hii
kwa kutoa mifano.
alama 20

SEHEMU YA D. USHAIRI

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Mbiu naipulizia, kwa wa hapa na ng`ambo,
   Kwaani ngoja `mesikia, inaumiza matumbo,
   Kwa upole sitafyoa, hata kama kwa kimombo,
   Yafaa jihadharia, maisha yas`ende kombo.

2. Maisha yas`ende kombo, kututoa yetu ari,
   Zingatia haya mambo, wetu walezi mukiri,
   Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri
   Watunzeni na maumbo, msijezusha hatari.

3. Msijezusha hatari, na nyingi hizi zahama,
   Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama
   Twaeleza kwa uzuri, matendoyo yatuuma
   Watoto tunayo mori, ni lini mtajakoma?

4. Ni lini mtajakoma, na pombe siso halali?
   Sio baba sio mama, mbona ny`hamtajali?
   Mwafaja nzi twasema, mwatuacha bila hali
   Hangaiko acha nyuma, kwani hamuoni hili?

5. Kwani hamuoni hili, kila saa mwapigana
   Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Mwatusumbua akili, twaumia ten asana
Acheni na ukatili, kwani upendo hamna.

6. Kwani upendo hamna, kama mbwa mwatuchapa
   Mwatuchoma sisi wana, mioyetu yatupapa
   Pa kujificha hatuna, tumebaki tukitapa

7. Tumevunjwa na mifupa, hata leo uke wetu,
   Mwatubaka na kuapa, kutung`ata nyi' majitu,
   Hayo makeke na pupa, mtakoma utukufu

8. Mtakoma utukufu, na kutumia mikiki
   Na tabia zenye kutu, tumechoka nayo chuki
   Hatutakubali katu, kutendewa yenye siki
   Serikali fanya kitu, kwani nasi tuna haki.

a. Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili.
   alama 2

.....
.

.....
.

b. Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili.
   alama 4

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

c. Taja nafsineni katika shairi hili.
   alama 1

.....
.

.....
.

d. Eleza bahari nne zinazowakilishwa katika shairi hili
alama 4

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

e. Andika ubeti wan ne kwa lugha nathari.
alama 4

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

f. Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili.
alama 3

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

g. Huku ukitoa mfano, taja mfano wa uhuru wa mshairi ambao ume tumiwa katika shairi hili. alama 2

.....
.

.....
.

.....
.

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Mlipozinduka,
Mkaungana na kushikana
Kwa nguvu moja mkavuta, mkavuta
Mdogo akivuta na mkubwa anavuta, nyote mlipovuta
Si makubwa mlitenda!
Babu yangu kajiunga
Babu yako akaja Mmoja alipokohoa, mwenzake akampokea
Homa hiyo kaenea ja moto wa kiangazi
Mau mau wakazalika, nywele ndefu zilizosokotana
Si mkoloni aliondoka!

Ubinafsi upigiwa teke
Kimoja wakajiona
Wala
Si viungo tofauti vya mwili mmoja
Si taifa lilisimama!
Doa ikaitwa Dola
Na wimbo wa taifa, kitambulisho
Vazi la taifa kashonwa
Bendera ilipepea!

Mbona msambaratiko?
Sasa
Mbona wa kwenu tu?
Vicheko si vicheko, bashasha juu ya bashasha
Wa ndani busu moto moto
Wengine soma mgongo!
Na kuta wajijengea, za mawe na za miba
Taba samuyo hela ngapi, waso wakalipe?

Na ndimi zatema ndimi

Miale ya kuunguza!
Wakweapo ulingoni
Wagongesha huyu na yule
Viongozi maluuni, waajiri kikabila
Kiongozi maluuni, cheo wakweza kwa kabila
Maluuni maluuni
Adhabu zako za kikabila!
Twajenga ukibomoa, mzalendo sampuli gani?

Nyoyo zetu lako shamba
Wazichimbua hisia, na mashimo wapanda chuki
Fitina ndo maji yako, Wanyunyiza na kwa bidii
Tofauti za kikabila, na lawama mzomzo
Pindi uwakapo moto, huyoo watakomea!
Kiongozi maluuni.

a. Huku ukitoa mifano mwafaka,eleza sifa za shairi huru zinazojitokea katika shairi hili.
alama 6

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

b. Fafanua aina tatu zamsambaratiko unaozungumziwa katika shairi hili.
alama 6

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

c. Bainisha mbinu sita za kifasihi zinazojitokeza katika shairi hili.
alama 6

.....
.....
.....
.....
.....
.....

.....
.....
.....

d. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi hili alama 2
   i.Bashasha
   ii.sampuli

SEHEMU YA E. FASIHI SIMULIZI.

Katika jamii ya Itaso watoto pacha huchukuliwa kama mkosi. Kwa hivyo, hubidi sherehe maalum ifanywe ili kutakasa wazazi wa watoto hawa. Sherehe hii hufanyika siku tatu baada ya kuzaliwa kwa watoto mapacha.

a. Tambua kipera kinachodokezwa na maelezo haya na ukifafanua.
   alama 2

.....
.....
.....
.....

b. Fafanua umuhimu wa kipera cha fasihi ulichotambua katika (a)
   alama 8

.....
.....
.....
.....

.....
.
.....
.....

.....

.....

.....
.....
.....

c. Fafanua sifa zozote tano za soga.
alama 5

.....
.

.....

.....
.....

.....

.....
.

d. Ni changamoto zipi zinaweza kumkumba mtafiti akifanya utafiti wa soga nyanjani.
alama 5

.....
.

.....
.

.....
.

.....
.

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 5

102/1

INSHA

MUDA:SAA 1¾

1 Mhariri wa jarida la shule yako ameamua kuchapisha habari kukuhusu.Andika tawasifu juu ya maisha yako tangu utotoni utakayomkabidhi mhariri huyo.

2 Pendekeza njia za kukabiliana na ongezeko la visa vya utovu wa maadili miongoni mwa vijana katika jamii.

3 Andika kisa kinachooana na methali``mchelea mwana kulia hulia mwenyewe''

4 Andika insha itakayokamilika kwa maneno haya.Mshtakiwa alimwangalia hakimu kwa macho ya huruma,kisha akamwangalia mkewe na wanawe akatamani kuwaomba msamaha lakini hukumu ilikuwa imetolewa.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

KCSE PREDICTOR 5

KISWAHILI

102/2

MUDA:SAA 2 ½

1.UFAHAMU: (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Gari lake kuukuu lilikuwa linapambana na barabara yenye mashimo yaliyoshiba na kutapika maji ya mvua ambayo sasa ilikuwa inaanza kupusa.Japo daima alipambana na usukani kunako mashimo haya yaliyotosha kuitwa magenge, alishukuru kwa hali hii.Vipi angeweza kulidhibiti gari lake hili kwenye barabara iliyosakafishwa nayo ikahitimu? Magurudumu haya yaliyong'ara kama upara wa shaibu aliyekula chumvi hadi ikamwogopa yangetii uelekezi wake? Mara ngapi gari hili limetaka kumwasi barabarani?Haya yalikuwa baadhi ya maswali yaliyompitikia akilini. Hakujitakilifu kutaka **kuyapa mji** maana mara ile mawazo yake yalitekwa na kubwagwa katika nchi ya mbali – nchi ambayo sasa aliiona kama sinema akilini mwake.

Alipofika nyumbani aliliegesha gari lake na kufululiza ndani. Siku mbili zilikuwa zimepita akiwa pale kazini. Madaktari kama yeye hawakuwa wengi. Alikuwa miongoni mwa madaktari wenye ujuzi katika hospitali hii ya kitaifa.Wenzake wengi walikuwa wamehamia ughaibuni walikokwenda kutafuta maisha. Mshahara wao wa mkia wa mbuzi uliwasukuma na kuwatema nje ya nchi yao. Wengi wa waliohamia ng'ambo waliona vigumu kubaki katika ajira ambayo kivuno chake kilishindwa kumvusha mtu hata nusu ya kwanza ya mwezi. Malalamishi ya kulilia ujira wa heshima yaligonga kwenye masikio yaliyotiwa zege. Na kweli wanavyosema, mwenye macho haambiwi tazama.Basi walitazama hapana pale wakaona penye mianya ya matumaini, nao wakaiandama.

Hadi leo hii hamna la mno lililofanyika. Ndiyo maana Daktari Tabibu anarudi nyumbani tangu kuingia kazini hiyo juzi alfajiri. Hafanyi kwa kuwa katosheka, maana pia yeye ana dukuduku. Ana shaka ya mustakabali wake ikiwa mazingira ni haya kumsoza, maana umri nao unazidi kumla. Japo anatia na kutoa, mizani ya hesabu yake imeasi ulinganifu.

Daktari Tabibu ni mfungwa. Ametekwa na kuzuiwa kwenye kipenda na kuchukia mambo. Ni kama mti uliodumaa. Anatamani barabara nzuri za lami. Anatamani mshahara wa kumwezesha kukidhi mahitaji yake na kutimiza majukumu yake ya kimsingi. Jana amesema na rafiki yake aliye ng'ambo kwa simu ambayo sasa imetulia mkabala naye. Ingawa mwenzake huyu alikuwa mchangamfu na kumdokolea hali ya maisha ya kuridhisha kule ugenini kama vile wanataaluma kuenziwa,yapo vilevile yaliyomtia unyonge mwoyoni. Upweke ndio ulimtia **fukuto** kuu. Licha ya hela zote hizo za kupigiwa mfano, watu hawana muda wa kutembeleana na kujuliana hali au hata kukutana tu mkahawani wakashiriki mlo. Eti ni kila mtu na hamsini zake. Halafu ipo

changamoto ya hali ya hewa.Baridi ya ng'ambo haifanyi mzaha katika kumtafuna mtu. Ni hali tofauti na ile aliyoizoea.

Daktari Tabibu alizitia kauli za rafiki yake kwenye mizani ya moyo wake. Akawaza ikiwa kweli si bora kulemazwa na mzizimo ugenini badala ya kuishi katika kinamasi cha kuumbuliwa nyumbani. Kisha punde lilimjia wazo la marehemu nyanyake na wengine kama yeye waliofadhili masomo yake kupitia kwa serikali na njia ya kodi. Je si usaliti huu?Vipi aikimbie nchi kabla ya kuihudumia ilhali imemjenga hadi kuwa daktari? Na je wafanyakazi wake wa nyumbani watakwenda wapi? Atawaambiaje kuwa sasa hahitaji huduma zao kwa kuwa anakimbia nchi yake?

Mawazo yake yalikatizwa na simu iliyolia na kumshtua. Alipoitazama aliiona imeng'ara kwa mwangaza ulioweka wazi jina la mpigaji. Alifahamu kuwa leo hii tena dharura nyingine ilikuwa inamwalika hospitalini. Hapo ndipo alipoiinua ile simu tayari kusema na mwenzake upande wa pili.

"Haloo!" sauti nyororo kutoka upande wa pili iliita.

"haloo!"

"Naam!Dharura nyingine tena daktari.Unaombwa kuokoa maisha mengine tena!"

"Haya. Ila mwanzo nitahitaji kujimwagia maji,"na pale pale akaikata ile simu.

Daktari Tabibu aliingia hamamuni huku kajifunga taulo kiunoni tayari kuoga.Aliyafungulia maji lakini ule mfereji uligoma kutapika maji.Ulikuwa umekauka kabisa.Dakrari Tabibu aliduwaa pale.Aliufunga ule mfereji kabla ya kuiaga bafu.

14. Eleza sababu **nne** zinazowafanya wataalamu kuhamia nchi za nje. (alama 4)
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
15. "Hakuna masika yasiyokuwa na mbu." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hali ya waliohamia nga'ambo. (alama
    3)……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……

……
……
……

16. Fafanua athari **tatu** zinazoikumba nchi ya msimulizi kutokana na uhamiaji ng'ambo wa wataalamu. (alama 3)……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

17. Eleza mchango wa teknolojia kwa kurejelea kifungu. (alama 3)……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

18. Eleza maana za msamiati ufuatao kulingana na taarifa. (alama2)

r) Kuyapa mji
……
……
……

s) Fukuto
……
……
……

2 UFUPISHO (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Wakenya walipoipata katiba mpya waliidhinisha mfumo wa ugatuzi. Katika mfumo huu, mamlaka ya serikali kuu katika uongozi, usimamizi na utumiaji wa rasilimali za nchi hupunguzwa. Kiasi Fulani cha mamlaka hutwaliwa na maeneo ya ugatuzi. Suala hili halikuzingatiwa katika katiba ya awali ambapo mamlaka yote yalikuwa

mikononi mwa serikali kuu. Kutokana na upana na wingi wa maeneo, iliiwia vigumu serikali kuu kuhakikisha kwamba kulikuwa na usawa wa kimaendeleo katika sehemu nchini.

Kwa mujibu wa katiba mpya, serikali kuu haina budi kuyasaidia maeneo yote ya ugatuzi ili yaweze kujinyanyua kiuchumi na kuboresha hali za maisha za wakazi wake. Vilevile ni jukumu la kila eneo la ugatuzi kuweka mikakati madhubuti ili kuchunguza na kubainisha rasirimali zote katika maeneo husika. Hili litasaidia kufumba rasilimali ambazo zinaweza kuchangia katika ustawishaji wa maeneo haya. Maeneo haya pia yanatakiwa kutafuta mbinu zitakazofanikisha uzalishaji na utumiaji wa rasilimali hizi kwa njia endelevu. Mojawapo ya mbinu hizi ni uongezaji thamani katika rasilimali yoyote inayozalisha kwenye eneo mahususi.

Maeneo mengi ya ugatuzi nchini humu yanategemea kilimo cha ufugaji kama mhimili wa uchumi. Licha ya kuwa nguzo, kilimo hiki hakijawahi kupigiwa darubini vizuri kwa lengo la kukiimarisha ili kiwanufaishe wenyeji kikamilifu. Aghalabu wafugaji wengi huandama mbinu za jadi za ufugaji ambazo haziwahakikishii ongezeko la mapato.Isitoshe, wafugaji hawa wanakabiliwa na tatizo katika soko la mifugo ambapo wengi hupunjwa na matapeli. Pamoja na haya, baadhi ya wakazi huuza mifugo nje ya nchi wakiwa wazimawazima bila kuwazia matokeo ya kitendo hiki. Si ajabu kuwaona ng'ombe, ngamia, mbuzi na kondoo wakipakiwa kwenye malori na kusafirishwa nje ya nchi. Ukweli ni kwamba jambo hili ni hatari sana, si kwa uchumi wa maeneo husika tu, bali pia kwa Kenya kwa jumla. Hii ni kwa kuwa walionunua mifugo wazimawazima wanaweza kuhiari kutowachinja na badala yake kuwatumia kama mbegu kwani baada ya muda huenda wanaonunua mifugo wakijitosheleza na kukosa kununua mifugo wengine. Hali ikiwa hivyo, maeneo yaliyotegemea soko hili huenda yakalipoteza taratibu, na bila shaka kupoteza natija inayotokana na soko lenyewe.

Ili kudhibitisha hali hii, itakuwa bora ikiwa viwanda vya kuchinjia mifugo na kupakia nyama vitajengwa katika maeneo haya ya ugatuzi. Hili litawawezesha wakazi kuuza nyama badala ya kuuza mifugo wazimawazima. Fauka ya hayo maeneo haya yatajikinga dhidi ya kupoteza bidhaa zinazotokana na mifugo. Hizi ni kama vile ngozi, kwato na pembe ambazo bila shaka zina natija kuu. Ngozi kwa mfano, ni bidhaa muhimu sana katikasekta ya utengenezaji wa mavazi na mifuko. Viwanda vinavyotumia ngozi kama malighafi vikijengwa katika maeneo haya, wakazi wake watanufaika si haba. Madhalani, viwanda vya kutengenezea viatu, mishipi, mifuko na nguo vikianzishwa,wawekezaji watalazimika kuanzisha viwanda vingine tegemezi. Kathalika, ni dhahiri kwamba bidhaa zinazotokana na ngozi huhitaji kutiwa nakshi. Kuanzishwa kwa viwanda hivi basi kutazua haja ya kuanzishwa kwa viwanda vingine vya kutengeneza rangi, pamoja na maduka ya kuuza bidhaa zenyewe. Isitoshe, gundi ya kugandisha bidhaa hizi itahitajika, hivyo kusababisha haja ya kuanzishwa kwa kiwanda cha gundi. Matokeo ya shughuli hizi zote ni kuzalishwa kwa nafasi anuwaiza kazi kwa wakazi. Hili litakuwa na matokeo zaidi chanya, hususan kwa vijana. Badala ya kushiriki ulevi na burudani zinazowahatarisha, wataweza kujitafutia riziki katika viwanda hivi.

Juu ya hayo, mfumo wa ugatuzi utayaweza maeneo husika kuongeza thamani, utoaji wa huduma za kijamii na kuitawala kulingana na mahitaji ya maeneo haya. Ni muhimu hata hivyo kuzingatia kwamba kila eneo la ugatuzi lina upekee wake, navyo vipaumbele hutofautianakulingana na maeneo. Kuna yale ambayo yatasisitiza usalama, mengine ujezi na uimirishaji wa miundomusingi kama vile barabara, vituo vya afya na hata taasisi za elimu. La muhimu ni wakazi wa maeneo husika kubainisha ni lipi litatekelezwa kwanza.

Kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Kufanikiwa kwa mfumo wa ugatuzi kutategemea juhudi za kila mkazi wa eneo husika. Ni muhimu kila mkazi kujiona kuwa mmiliki wa eneo zima la ugatuzi na kuwajibika katika kuliendeleza kwa hali na mali.uwajibikaji huu unajumuisha uteuzi wa viongozi wenye muono mzuri na ambao

utawawezesha kuyafikia malengo yao ya kimaendeleo. Hakika, mustakabali na uwepo wa eneo la ugatuzi utakuwa zao la maamuzi ya wanaeneo. Vilevile ufanisi wa maeneo ya ugatuzi utakuwa msingi wa ufanisi wa taifa kwa jumla.

iii) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 85-90 (alama 8, 1 mtiririko)

Matayarisho:……

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

Nakala safi:

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

iv) Kwa kutumia maneno 75-80, bainisha masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama7, 1 mtiririko)

Matayarisho:……

……
……
……
……

……
……
……
……
……
……
……
……

Naala safi:……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

3.MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

h) i) Andika tofauti moja kati ya sauti zifuatazo. (al2)

iii) |ng'| na |gh|

……
……
……
……
……
……

iv) |v| na |f|

……
……
……
……

v) |r| na |l|

……
……

……
……

vi) |m| na |n|

……
……
……
……

i) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi : O (al 2)

……
……
……
……
……

j) Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U – ZI (al2)……
……
……
……
……

k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa. (al 2)

Ngoma hizo zao ziliibwa na wezi wale.

……
……
……

l) Tumia ‘kwa’ katika sentensi kuonyesha :

9. Sehemu ya kitu kizima (al2)

……
……
……

10. Namna tendo lilivyofanyika (al2)……
……
……

m) Bainisha maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo (al2)

Bedui

alimrushiatufe.

……
……
……
……
…

g) Andika visawe vya maneno yafuatayo (al2)

i) Doa ……..

ii)Omba ……

3. Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya rithi na ridhi (al2)……
……
……

4. Bainisha silabi katika neno:

Wanyweshavyo (al1)

5. Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo (al2)

Mwenyewe alikipenda kwa dhati.

……
……
……
……
……

6. Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (al2)

Mkihifadhi nafaka hizo vizuri maeneo haya yatakuwa na vyakula vya kutosha.

……
……
……

7. Andika neno moja lenye mofimu zifuatazo:

nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita, yambwa, mzizi, kauli ya kutendesha ,kiishio kutenda.(al2)

……
……
……
……
…….

8. Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi (al 4)

Lililimwa vizuri sana.

9. Kanusha sentensi ifuatayo.

   Wanafunzi waliingia darasani wakatoa vitabu wakaanza kusoma.(al2)

   ……
   ……
   ……
   ……
   ……

10. Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (al2)
    i) Furaha-
       ……
       ……
       ……
    ii) Nyasi-
       ……
       ……
       ……

11. Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya nukta pacha. (al2)

    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……
    ……

12. Andika sentensi ifuatayo upya ukianzia kwa yambwa tendwa (al2)

    Wafugaji waliwakatia ng'ombe wote majani ya mti huo.

    ……
    ……
    ……

13. Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (al2)

Ingawa mshahara wake si mkubwa anaikimu familia yake.

14. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo: (al2)

Watoto wameombwa waanike nguo.

……
……
……

15. i) Eleza maana ya shadda (al1)

……
……
…….

ii)Onyesha panapotokea shadda katika neon:

mteremko. (al1)

……
……
……..

ISIMU JAMII (ALAMA10)

…….watu wakaunti ya Cheneo wamesahaulika kabisa Ningependa kuelezwa kinaga ubaga kama hawa ni wakenya au la. Order! Order! Mheshimiwa Kega.

c) Hii ni sajili gani? (al2)

……
……
……

Eleza sifa nane za sajili iliyotajwa. (al 8)

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

KCSE PREDICTOR 5

102/3
KISWAHILI
FASIHI YA KISWAHILI

MUDA: SAA $2^1/_2$

1.SEHEMU A: USHAIRI (LAZIMA)

Eti
Mimi niondoke hapa
Niondoke hapa kwangu
Nimesaki, licha ya risasi
Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi
Siondoki
Siondoki siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Kwa mateke hata na mikuki
Marungu na bunduki, siondoki

Hapa
Siondoki
Mimi ni Pahame!
Niondoke hapa kwangu!
Fujo na ghasia zikizuka
Na kani ya waporaji, siondoki

Haki
Siondoki
Kwangu siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Nawaje; waje wanaokuja
Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe
Siondoki
Ng'oo hapa kwangu!
Katizame chini mti ule!
Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi
Nende wapi?
Si hapa kitovu changu

Niondoke hapa kwangu
Wangawa na vijikaratasi
Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu
Siondoki
Sihitaji karatasi
Niondoke hapa kwangu
Yangu mimi ni ardhi hii
Wala si makaratasi, siondoki

Maswali

a) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini (alama 2)

b) Taja masaibu anayopitia mzungumzaji (alama 4)

c) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)

e) Tambua matumizi ya mbinu ya usambamba (alama 2)

f) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)
g) Tambua idhini moja ya mtunzi (alama 1)
h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (alama 3)
(i) Karatasi
(ii) Nimesaki
(iii)kitovu

2<u>SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOGO</u>

2.Uliona nini kwa huyo zebe wako ? Eti mapenzi!

1. Eleza muktadha wa dondoo. (al. 4)
2. Andika mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili (al. 4)
3. Taja hulka za mnenaji unajitokeza katika dondoo. (al. 2)
4. Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirekjelea tamthilia. (al. 10)

3.wa kurejelea tamthlia ya 'Kigogo ya Pauline Kea, onyesha jinsi ambavyo viongozi wengi katika nchi za kiafrika wamejawa na tamaa. (alama 20)

SEHEMUC.RIWAYA YA CHOZI LA HERI(ASSUMPTA MATEI)

4.“ Kwa kweli ni hali ngumu hii”
Weka dondoo katika muktadha wake. (alama4)
Ni hali gani yamsemewa inayorejelewa kwenye dondoo. (alama16)

5) Ukabila ni tatizo sugu katika nchi nyingi za Kiafrika. Tetea kauli hii ukilejelea Chozi la Heri (al. 20)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine
jibu swali la 6 au la 7

6.Ukirejelea hadithi zifuatazo, eleza jinsi maudhui ya mapenzi na asasi ya ndoa yanavyojitokeza. (alama20

a) Mapenzi ya kifaurongo
b) Masharti ya kisasa
c) Ndoto ya Mashaka
d) Mtihani wa maisha

Au

Shibe inatumaliza : Salma Omar Hamad

7.“Hiyo ni dharau ndugu yangu. Kwa nini kila siku tunakula sisi kwa niaba ya wengine ?”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b)Eleza sifa za msemaji. (alama 6)
c) Eleza jinsi viongozi wanavyokuwa wabadhirifu. (alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8a) Fafanua mchakato/fomula ya uwasilishaji wa vitendawili. (alama4)
b) Linganisha naulinganue vitendawili na methali. (alama10)
c) Toa sababu sita za kudidimia kwa fasihi simulizi. (alama6)

KCSE PREDICTOR 6

KISWAHILI 102/1
Karatasi ya 1
INSHA
MUDA: Saa 1 ¾

MASWALI

LAZIMA

1. Wewe kama rais umekerwa na kukithiri kwa ufisadi katika wizara mbalimbali. Andikia arifa mawaziri wako ukiwaeleza madhara ya ufisadi na hatua utakazochukua ikiwa hawatakomesha ufisadi katika wizara zao. (alama 20)

2. Dhuluma katika asasi ya ndoa haiathiri tu wanajamii husika nyumbani bali elimu ya watoto wao pia. Fafanua. (alama 20)

3. Andika kisa kinachoafiki methali:…. Usishindwe kupika ukasingizia jiko la moshi. (alama 20)

4. Andika insha itakayokamilika kwa maneno yafuatayo:
…….Ni jicho gani lisilolengwalengwa na chozi la mshangao na huzuni kwa kushuhudia unyama wa aina hii. Wanadamu wamesahau kuwa mtu ni utu. (alama 20)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

KCSE PREDICTOR 6

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
Muda: Saa 2 ½

1. UFAHAMU: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Mawasiliano ni upashanaji habari kwa namna tofautitofauti. Njia za mawasiliano zimebadilika sana katika historia ya binadamu. Kwa mfano, zamani ingechukua siku nyingi kupitisha ujumbe baina ya watu wanaoishi sehemu mbalimbali. Siku hizi ujumbe hupitishwa katika sekunde chache katika masafa marefu.

Ugunduzi wa simu uliofanywa na Alexander Graham Bell mwaka wa 1876 ulifungua ukurasa mpia katika mawasiliano. Nchini Kenya, miaka ya sabini na themanini, ilikuwa vigumu kupata huduma za simu. Mtu alihitajika kusafiri masafa marefu ili kupata huduma hizo hasa kwa wale walioishi mashambani. Aidha kutokana na ukosefu wa huduma hizo katika sehemu nyingi, mtu alihitaji **kupiga foleni** ili ahudumiwe ama ajihudumie.

Baadaye, simu tamba zilivumbuliwa na mawasiliano yakarahisishwa. Mwanzoni, simu tamba zilikuwa vidude vikubwa ambavyo havikutoshea mifukoni. Hata hivyo, usumbufu huo ulitafutiwa suluhu. Siku hizi simu tamba ni ndogo na hivyo huwa rahisi kuzibeba. Aidha, kampuni za kutoa huduma za mawasiliano na kufanya gharama ya kupiga simu kuenda chini.

Barua pia ni njia ya mawasiliano na imetumika kwa muda mrefu. Baadhi ya nchi kuliko tumiwa barua katika enzi za zamani ni Misri na Uyunani. **Matarishi** walitumwa kupeleka barua. Barua zilichukua muda mrefu kufikia aliyeandikiwa. Aidha kutokana na kwamba si watu wote waliojua kusoma na kuandika, wachache waliokuwa na maarifa hayo waliwandikia na kuwasomea. Katika enzi hizi matumizi ya barua yamepunguzwa kwa kiwango kikubwa na tarakilishi na simu tamba. Kwa kutumia tarakilishi unaweza kutuma barua pepe. Aidha, kwa kutumia simu tamba unaweza kutuma arafa.

Waajiri wengi hupendekeza wanaoomba kazi watume maombi yao kwa kutumia baruapepe. Njia hii huondoa uwezekano wa wanaoomba kazi kutumia ufisadi ili wapate kazi. Aidha, njia hii husaidia kutunza mazingira kwani karatasi hazitumiwi. Katika elimu tarakilishi zinatumiwa shuleni kufundishia hivyo kurahisisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Aidha, kupitia tarakilishi iliyotandawizwa ama kuunganishwa kwa mtandao, watu huweza kujuliana hali na kupashania habari mbalimbali kutoka pembe zote za dunia. Changamoto katika hatua hii ni ukosefu wa nguvu za umeme hasa mashambani. Aidha,gharama ya kununua tarakilishi ni kali mno hasa kwa mataifa yanayoendelea ikizingatiwa kuwa yana changamoto za kimsingi kama vile kutojua kusoma na kuandika, magonjwa na umaskini.

Vilevile, redio ni chombo muhimu ambacho huchangia sana katika mawasiliano. Kwa sasa, hiki ndicho chombo cha pekee kinachomilikiwa na karibu kila familia. Hali hii inachangiwa na ukweli kwamba kunazo redio ndogo ambazo hutumia betri. Chombo hiki huwapitishia matangazo na habari kuhusu yanayotendeka kutoka pande zote za ulimwengu. Redio hufahamisha, huburudisha na kuelimisha. Wizara ya Elimu imekuwa ikitumia redio kufundishia masomo mbalimbali hasa katika shule za msingi.

Nani asiyejua kuhusu runinga? Chombo hiki pia hutoa mchango mkubwa katika mawasiliano. Runinga hushirikisha hisi za kusikiliza na kuona, kwa hivyo mawasiliano yake hufanikiwa sana. Hata hivyo, ni asilimia ndogo ya watu ambao wanaweza kuimiliki kutokana na gharama yake na pia si wengi wanazo nguvu za umeme majumbani mwao.

Mwalimu ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii oyote. Ni dhahiri shahiri mwasiliano ni sehemu muhimu katika kuimarika kwa uchumi. Vile vile huwezesha watu kutangamana na kubadilishana mawazo. Binadamu si kama visiwa vinavyosimama peke yavyo. Binadamu huhitaji kutangamana na binadamu wengine katika maisha na kwa hivyo mawasiliano ni muhimu.

a) Eleza kini cha taarifa hii. (al. 1)

……

……

……

……

b) Toa sababu mbili za waajiri kuhimizi matumizi ya barua pepe. (al. 2)

……

……

……

……

……

c) Kwa nini redio ndicho chombo kinachotegemewa zaidi katika mawasiliano.
Eleza sababu nne. (al. 4)

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

d) Kwa mujibu wa kifungu hiki eleza udhaifu wa tarakilishi. (al. 3)

……

……

……

……

……

……

……

……

e) Eleza faida mbili za tarakilishi. (al. 2)

……

……

……

……

……

……

……

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (al. 2)

i) Kupiga foleni

……

…

ii) Matarishi

……..

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali yafuatayo

Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumzo.

Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza kama vila michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidia katika

maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile ilivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amefiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati juao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambae amepatikana na mambo kama huyo hana budi kufahamu zaidi.
Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo , karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.
Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza . Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65 (alama 10, 1 ya utiririko)
Matayarisho

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

Jibu

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho (Maneno 30) (alama 5 utiririko)

Matayarisho

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

……
……

Jibu

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vielezi viwili vya silabi moja. (al. 2)

……
……
……
……
……
……

b i) Eleza maana ya sauti za likwidi. (al. 1)

……
……
……

ii) Toa mifano ya sauti za likwidi. (al. 1)

……
……
……

c) Ainisha mofimu: Lililoliwa (al. 3)

……

……

……

……

……

……

……

d) Eleza huku ukitoa mifano matumizi mawili ya kiambishi ‘ji’. (al. 2)

……

……

……

……

……

……

e) Huku ukionyesha upatanisho wa kisarufi katika sentensi, weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka. (al. 2)

i)

Uwele……

……...…

……

……..…

ii) Vita

……

……..……

……

……..……

f) Tumia ‘O’ rejeshi tamati kuunganisha sentensi zifuatazo. (al. 1)

Tawi limekauka
Tawi limeanguka

……

……

……

……

……

g) Tambua vivumishi na uonyeshe ni vya aina gani. (al. 3)

Wanafunzi wawa hawa waliochelewa watafanya kazi ya sulubu kama adhabu.

……

……

……

……

……

……

……

h) Kanusha: Msichana ambaye amefika ametuzwa. (al. 1)

……

……

……

i) Onyesha aina za virai katika sentensi hii: (al. 2)

Wale wazazi wetu watawasili kesho saa tatu.

……

……

……

……

……

……

……

j) Unda nomino kutokana na kitenzi ‘Haribu’ (al. 1)

……

……

……

……

……

k) Tambua aina za vitenzi katika sentensi. (al. 2)

Hawa sio wachezaji bali wamekuwa wakichezea timu hii.

……

……

……

……
……
……
……

l) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya viunganishi vya kulinganua. (al. 1)

……
……
……
……
……

m) Eleza matumizi mawili ya ‘ka’ . Toa mifano katika sentensi. (al. 2)

……
……
……
……
……
……
……
……

n) Andika visawe ya maneno yafuatayo (al. 2)

i) Daawa

……
……..

ii) Ainisha

……
……..

o) Onyesha kwa kauli ulizopewa (al. 1)

i) Ja (tendewa)

……

……

……

p) Andika kinyume: Tajiri aliyesifiwa amelaaniwa. (al. 1)

……

……

……

q) Chananua sentensi hii kwa kutumia vishale. (al. 4)

Yule mgeni aliyefika jana ameondoka leo.

……

……

……

……

……

……

……

……

……

r) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (al. 2)

Oyula atapendwa na wengi ikiwa atashinda leo.

……

……

……

……

……

s) Eleza majukuma mawili ya chagizo huku ukitoa mifano. (al. 2)

……

……

……

……

t) Akifisha. (al. 3)

sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote kumbuka

……
……
……
……
……
……
……

u) Andika ukubwa wa sentensi katika wingi. Nyundo imo ndani ya kibweta. (al. 1)

……
……
……

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) Eleza matatizo matano yanayowakabili wazungumzaji wa Kiswahili. (al. 10)

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 6

102/3

KISWAHILI YA 3.

FASIHI.

MUDA : SAA 2 ½

SEHEMU A : RIWAYA – LAZIMA

1. Fafanua ufaafu wa anwani ‘Chozi la Heri’ (al. 20)

SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOGO

2. Uliona nini kwa huyo zebe wako ? Eti mapenzi!

i) Eleza muktadha wa dondoo. (al. 4)

ii) Andika mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili (al. 4)

iii) Taja hulka za mnenaji unajitokeza katika dondoo. (al. 2)

iv) Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirekjelea tamthilia. (al. 10)

Au

3. Ni bayana kwamba viongozi wengi nchi zinazoendelea wamejawa na tama na ubinafsi. Thibitisha kaul hi ukirejelea tamthilia Kigogo (al. 20)

4.

SEHEMU C: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI ZINGINE

SHIBE INATUMALIZA

5. “Ndugu yangu kula kunatumaliza”
   “Kunatumaliza au tunakumaliza”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

b) Fafanua maana kitamathali katika kauli ‘Kula tunakumaliza’ (al. 10)

c) Kwa mujibu wa hadithi hii, kwa namna gani wasemaji wanadai kula kunawamaliza? (al.6)

Au

a) ‘MAME BAKARI’

Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake, onyesha kwa mifano mwafaka. (al. 10)

b) ‘MASHARTI YA KISASA’

“..... mapenzi ni mateso, ni utumwa, ni ukandamizaji, ni ushabiki usio na maana.”

Thibitisha ukweli wa kauli hii kama unavyojitokeza kwenye hadithi. (al. 10)

SEHEMU D : USHAIRI A

6. MWANA

1. Kwani mamangu u ng’ombe, au u punda wa dobi ?
   Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi
   Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi
   Hebu nambie
   Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

MAMA

2. Nang’ona mwana nang’ona, sitafute angamiyo
   Sinipe kuja sonona, kwa uchungu na kiliyo
   Babayo mkali sana, kubwa pigo la babayo
   Kwani kelele kunena, huyataki maishayo ?
   Hilo nakwambia.

MWANA

3. Sitasakamwa. Kauli, nikaumiza umiyo
   Nikabeba idhilali, nikautweza na moyo

Siuvuwati ukweli, hazidisha gugumiyo
Baba hafanyi halali, huachi vumiliyo
Hebu nambie.
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Nambie ipi sababu, ya pweke kwenda kondeni
Nini yako matulubu, kulima hadi jioni ?
Na jembe ukudhurubu, ukilitua guguni
Yu wapi wako muhibu, Baba kwani simuoni?
Hebu nambie.
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Baba kwani simuoni, kuelekea shambani?
Kutwa akaa nyumbani, na gumzo mitaani.
Hajali hakudhamini, wala haoni huzuni.
Mwisho wa haya ni nini ? ewew mama wa imani ?
Hebu nambie.
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Na kule kondeni kwako, ukate kuni kwa shoka
Ufunge mzigo wako, utosini kujitwika
Kwa haraka uje zako, chakula upate pika
Ukichelewa vituko, baba anakutandika
Hebu nambie.
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Chakula kilicho ndani, ni jasho lako hakika
Kiishapo u mbioni, wapiti kupokapoka
Urudi nje mekoni, uanze kushughulika
Ukikosa kisirani, moto nyumbani wawaka
Hebu nambie.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

MAMA
Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka
Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka
Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka
Ninaanza kijipanga, kwa mapambano hakika
Hilo nakwambia

MASWALI

a) Mtunzi wa shairi hili alikuwa na dhaimira gani katika kutunga shairi hili (al. 2)
b) Shairi hili ni la aina gani. Toa ithibati (al. 2)
c) Yataje mambo yoyote matano anayolalamikia mwana (al. 5)
d) Eleza kanuni zilizotumika kasarifu ubeti wa tatu (al.5)
e) Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi (al. 4)
f) Eleza maana haya yaliyotumika katika shairi hili
   i) Jaza (al. 1)
   ii) Muhibu (al. 1)

7. <u>SHAIRI B</u>

Soma shairi hili kisaha ujibu maswali

1. Punda kalibebe gari, gari limebeba punda.
   Mwalimu ana pakari, muashi vyuma adunda
   Jaji gonga msumari, sonara osha vidonda
   Kinyume mbele.

2. Saramala ahubiti, muhunzi tiba apenda
   Mganga anabiri, baharini anakwenda
   Hata fundi wa magari, anatomea vibanda
   Kinyume mbele

3. Wakili anahiyari, biashara kuitenda
   Mtazame askari, akazakaza kitanda,
   Mkulima mashuhuri, jembe limemshinda
   Kinyume mbele

4. Apakasa daktari, ukili anaupinda
   Seveya kawa jabari, mawe anafundafunda,
   Hazini wa utajiri, mali yote aiponda,
   Kinyume mbele

5. Msemi huwa hasemi, wa inda hafanyi inda
   Fahali hawasimami, wanene walishakonda
   Walojitia utemi, maisha yamewavunda
   Kinyume mbele

6. Kiwapi cha kukadiri, twavuna shinda kwa shinda
   Tele haitakadiri, huvia tulivyopanda
   Mipango nmehajiri, la kunyooka hupinda
   Kinyume mbele

MASWALI

a) Mtunzi aliuwa na malengo gani alipotunga shairi hili? (al. 3)
b) Licha ya tarbia, eleza bahari nyingine zinazojitokeza katika shairi hili. (al. 4)
c) Eleza namna mtunzi alivyotumia uhuru wake. (al. 5)
d) Ni mbinu gani inayotawala shairi hili? (al. 2)
e) Uandike ubeti wa nne katika lugha nathari (al. 4)
f) Eleza toni ya shairi hili (al. 2)

SEHEMU E

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

7. FASIHI SIMULIZI

1. Eleza vigozi vinne vya kuandika methali (al. 4)
2. Eleza fani zinazozijenga vitendawili vifuatavyo (al. 4)
   i) Ajenga ingawa hana mikono
   ii) Jani la mgomba laniambi habari zinazotoka ulimwenguni kotew
3. Nini tofauti kati ya misimu na lakabu ? (al. 2)
4. I) Miviga ni nini ? (al. 2)
   ii) Fafanua hasara zozote tano za miviga (al. 5)
5. I) Tambua kipera cha maka yafuatayo (al. 2)
   " Wewe ni mbumbumbu kiasi kwamba ukiona picha yako kwenye kioo unashangaa ulimwona wapi mtu huyo".
   i) Ngomezi ni nini? (al. 1)

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 7

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

MUDA: SAA 1 ¾

INSHA

SWALI LA LAZIMA

1. Kama mhariri wa gazeti, andika **tahariri** ukipongeza hatua ya serikali kupiga marufuku matumizi ya karatasi za sandarusi.

CHAGUA MOJA:

2. Eleza njia za kustawisha uchumi uliosambaratika katika eneogatuzi lako.
3. Pwagu hupata pwaguzi.
4. **Andika** insha itakayomalizikia kwa maneno haya.

   "…Nilipokaa mezani kula chakula kitamu, nilikumbuka maisha magumu niliyoyapitia, nikatambua kuwa si rahisi kupata chakula kama hicho bila juhudi maishani"

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

KCSE PREDICTOR 7

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA 2

MUDA: SAA 2 ½

1. **UFAHAMU:** **(ALAMA 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi – vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitisha hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao

masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahabu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kinga zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na, ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

Maswali

a) Yape makala haya kichwa. (alama 2)

……

……

……

b) Mbali na athari kwa uzazi kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. (alama3)

……

……

……

c) Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. (alama 4)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

……

……

……

……

(d) Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu. (alama 2)

……

……

……

……

(e) Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. (alama 3)

……

……

……

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa. (alama 1)

Gandwa

_____

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali:

Biashara ya kimataifa ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile. Nchi mbalimbali zimekuwa zikitegemeana kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, nchi ya Kenya imekuwa ikiuza maua na mboga katika nchi za ng'ambo na kupata fedha za kigeni ambazo hutumiwa humu nchini kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Biashara ya kimataifa huziwezesha nchi ambazo hazizalishi bidhaa na hata huduma mbalimbali kupata bidhaa hizo kutoka nchi nyingine zinazohusiana nayo katika biashara. Mathalan, Kenya ni nchi ambayo imekuwa ikitegemea kilimo lakini haijaendelea katika sekta ya viwanda. Kenya huagiza bidhaa kama vile vipuri vya magari na hata magari yenyewe kutoka nchi kama vile Japan. Nayo Kenya huuza mazao ya shambani kama vile pareto, chai na kahawa ng'ambo.

Kupitia kwa biashara ya kimataifa, nchi hupata masoko kwa bidhaa zake. Kwa vile biashara ya kimataifa huziwezesha nchi husika kuzalisha bidhaa mahususi ambazo

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

hazitaigharimu nchi pesa nyingi kuzalisha, nchi hizo aghalabu huzalisha kiasi kikubwa cha bidhaa kuliko mahitaji yake ya nyumbani. Nchi basi hulazimika kutafuta masoko nje ya mipaka yake. Kwa njia hii uchumi wa nchi huendelea kuimarika.

Aidha, biashara ya kimataifa huwezesha nchi kupata huduma za kitaaluma ambazo hazipatikini katika nchi husika. Kuna nyanja za kiuchumi ambazo huhitaji wataalamu mahususi. Kwa mfano, katika sekta ya matibabu nchini humu tumepata kwamba kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanahitaji matibabu maalumu. Wanaougua magonjwa haya huagiziwa madaktari kutoka ng'ambo au hata kupelekwa ng'ambo kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

Biashara ya kimataifa hukuza ushirikiano wa kimataifa. Nyakati za majanga ya kimaumbile na hata mengine yanayosababishwa na kutowajibika kwa binadamu, nchi hupata usaidizi kutoka nchi za ng'ambo. Kwa mfano wakati wa mkasa wa bomu wa 1998, Kenya ilipata msaada wa kukabiliana na janga hili kutoka Israeli, Marekani na hata Ujerumani ambako baadhi ya waathiriwa wa mkasa huo walipelekwa kwa matibabu zaidi. Ushirikiano huu wa kimataifa huwezesha wananchi kutoka nchi fulani kwenda kusomea na hata kufanya kazi katika nchi nyingine. Katika miaka ya hivi karibuni Wakenya wengi wamekuwa wakienda kusomea vyuo vikuu vya ng'ambo. Wengine wamediriki kupata kazi katika mashirika ya kimataifa katika nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Rwanda, Msumbiji na kadhalika.

Biashara ya kimataifa husaidia kukuza ushindani kati ya nchi husika. Ushindani huu ni hakikisho la uzalishaji wa bidhaa za thamani bora. Kila nchi itafanya juu chini kuzalisha bidhaa ambazo zinaweza kukubalika katika soko la kimataifa. Pia wananchi wa nchi husika hupata aina tofauti za bidhaa badala ya kutegemea aina moja tu ya bidhaa zinazozalishwa nchini mwao.

Biashara ya kimataifa huleta ushirikiano wa kisiasa na uelewano zaidi kati ya madola mbalimbali. Mathalan muungano wa nchi za Afrika Mashariki – Kenya, Uganda na Tanzania, hauchangii tu kuleta manufaa ya kiuchumi bali huleta ushirikiano zaidi wa kisiasa.

Ingawa biashara ya kimataifa ina natija, biashara hii huandamana na hasara mbalimbali. Biashara hii imesababisha kuwapo kwa masoko huru ambayo yameleta ushindani mkubwa kwa wafanyibiashara wadogo wa humu nchini. Baadhi ya wafanyibiashara wamelazimika kufunga biashara zao baada ya kufilisika. Ushuru mkubwa unaotozwa baadhi ya bidhaa nchini huwafanya wananchi wengi kutofaidika kwa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, kuna ucheleweshaji wa bidhaa zilizoagizwa. Bidhaa hizi mara nyingi huchukua muda kabla ya kutoka nchini, kwa hivyo wafanyibiashara wengi hulazimika kungojea kupata bidhaa hizi na kuwauzia wateja wao.

Vilevile, kutokana na biashara ya kimataifa, bidhaa duni huweza kupenyezwa katika mataifa yanayoendelea. Pia baadhi ya wafanyibiashara wa kimataifa huchukua fursa hii kulangua dawa mbalimbali za kulevya ambazo huwaathiri vijana wa nchi husika. Wengine huhusika katika vitendo vya kigaidi kama vile uchomaji wa majengo mbalimbali kwa bomu na mauaji ya ananchi wasio na hatia.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Ni kweli kuwa biashara ya kimataifa ina hasara zake. Hata hivyo mhimili mkubwa wa uchumi wa mataifa machanga.

(a) Kwa maneno yasiyozidi **themanini**, eleza umuhimu wa biashara ya kimataifa.(alama 7)

Matayarisho

……
……
……
……
……
……Nakala safi
……
……
……
……
……
……
……

(b) Kwa maneno yasiyozidi **40**, eleza ujumbe wa aya tatu za mwisho. (alama 6)

Matayarisho

……
……
……
……
……
……
……Nakala safi
……
……

……
……
……
……

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) Sahihisha sentensi: (alama 2)

(i) Mitume hiyo siyo ambayo tunaijua.

……

(ii) Wasikilizaji sasa wanaburudika na muziki kutoka idhaa la taifa hii.

……

(b) Ikanushe sentensi hii katika umoja. (alama 2)

Wasingecheza kiustadi wasingeshinda katika michezo ile.

……

(c) Tambulisha nyakati na hali katika sentensi: (alama 2)

(i) Wachezaji walikuwa wanafanya mazoezi.

……
……...

(ii) Nkirote alipoingia alitukemea.

……
……

(d) Eleza maana za sentensi. (alama 2)

(i) Kwa nini wasililie hapa?

……
……...

(ii) Kwa nini wasilie hapa?

……

……

(e) Toa mifano miwili miwili ya sauti zinazotamkiwa katika : (alama 2)

(i) ufizi ……

(ii) meno ……

(f) Andika udogo na ukubwa wa neno ‘kidole’. (alama 2)

(i)……(ii)……

(g) Tunga sentensi mbili tofauti kubainisha matumizi ya KWA. (alama 2)

(i)……

(ii)……

(h) Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Msichana alimkaririra mgeni shairi.

(i) ……

(ii)……

(i) Tumia vitenzi hivi katika sentensi mojamoja katika jinsi ya kufanyiwa. (alama 2)

(i) nywa

……

(ii) pa

……

(j) Kistari kifupi (-) aghalabu hutumika kuendeleza sauti hasa katika vihisishi. Onyesha matumizi mengine matatu ya alama hii akifishi. (alama 3)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

(i)…….

(ii)……

(iii)……

(k) Tunga sentensi kubainisha tofauti kimaana kati ya vitawe: (alama 2)

(i)juha……

(ii)jua……

(l) Ziandike upya sentensi hizi kwa mujibu wa maagizo uliyopewa. (alama 2)

(i) Kiyondi aliukomelea mlango alipovisikia vishindo.

(Anza kwa :Mlango……..)

……

……

(ii) Mvua ilinyesha sana alasiri hiyo. Wachezaji walicheza mpira vizuri tu.

(Tumia 'japo')

……

……

(m) Tunga sentensi sahihi kubainisha matumizi ya KI kuonyesha: (alama 4)

(i) masharti

……

(ii) ngeli

…….

(iii) kufanyika vitenzi viwili au zaidi wakati mmoja

……

(iv) kielezi namna

……..…

(n)Tambua hali na matumizi ya kisarufi ya neno lililopigwa mstari katika sentensi: (alama 1)

Mtu <u>mzee</u> anapaswa kuheshimiwa

……

(o) Andika katika usemi halisi. (alama 2)

Mwalimu aliwaagiza wanafunzi warudi darasani, warejelee madaftari yao ya kumbukumbu na kuikosoa kazi hiyo.

……
……
……..……
……..

(P) Andika katika umoja. (alama 2)

Tembe ambazo tulizimeza zilikuwa chungu.

……

(q) Eleza maana za semi au nahau: (alama 2)

(i) kwenda mbweu

……
……

(ii) shika sikio

……
……

(r) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali (alama 4)

Kiatu kilichonunuliwa juzi kimerejeshwa dukani

4. ISIMU - JAMII

(a) Eleza ukionyesha bayana tofauti baina ya lahaja na lafudhi. (alama 4)

……

……

……

……

……

……

(b) Taja sifa tatu tambulizi za lugha ya misimu (alama 3)

……

……

……

……

(c) Orodhesha sifa kuu za sajili ya siasa. (alama 3)

……

……

……

……

……

……

……

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 7

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI

MUDA: 2 ½
SWALI LA LAZIMA

1.HADITHI FUPI **ALAMA 20**

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE :Alifa Chokocho Na Dumu Kayanda

Mtihani wa Maisha

1. *"..Acha nijiondokee duniani niwaachie wafanisi wafanikie."*
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. Alama 4
   b) Taja na ufafanue sifa tatu za msemaji. Alama 6
   c) Eleza jinsi maisha ya msemaji yanavyoafiki anwani ya hadithi. Alama 10

2.RIWAYA CHOZI LA HERI : Assumpta Matei **ALAMA 20**

2. Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya Chozi la Heri. Alama 20
3. *"...liandikwalo ndilo liwalo? Since when has man ever changed his destiny?"*
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. Alama 4
   b) Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. Alama 6
   c) Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, **" liandikwalo ndilo liwalo''**, inavyojitokeza katika Chozi la Heri. Alama 10.

3.TAMTHILIA KIGOGO : Pauline Kea **ALAMA 20**

4. "Utawala wa Majoka katika jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyoka." Jadili. Alama 20
5. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika tamthilia ya Kigogo
   i) Kinaya Alama 6
   ii) Majazi Alama 8
   iii) Jazanda Alama 6

4.FASIHI SIMULIZI **ALAMA 20**

6. a) Eleza **aina** tano za wahusika wa fasihi simulizi. Alama 10

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

b) Eleza sifa za wahusika wa mighani. Alama 10

7. a) Eleza namna amabavyo hadhira wanahusishwa katika utambaji.Toa hoja nne. Alama 8

b) Taja na ueleze sifa nne bainifu za hadithi. Alama 4

c) Taja viungo vinavyopambanua muundo wa nyimbo katika jamii Alama 4

d) Andika majukumu manne ya nyimbo katika jamii Alama 4

5.USHAIRI ALAMA 20

8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Zitavuma,
Zitakoma,
Nitakwima,
Mti-mle.

Na muda nikisimama,
Nitatongoa nudhuma,
Kwa tenzi zilizo njema,
Nilisifu mti – mle.

Tazipanga tathlitha, tungo zilizo na hekima,
Za huba na thiatha, za kuburudi mitima,
Mashairi mabuthutha, musome mnaosoma.

Mti nishainukia,namea kuwa mzima,
Mizizi yadidimia, ardhini imeuma,
Nanena kitarbia, tungo zilizo adhama
Japo ni tungo za zama, mti-mle hutumia.

Zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,
Dharuba kinitikisa, mti-mle huinama,
Huyumba nikaziasa, matawi yakakingama,
Gharika ikishapisa, hurudi nikawa wima,
Na tungo za takhimisa, mti-mle huzipima.

Maswali

(a) Shairi hili ni la kimapokeo. Toa sababu mbili **kuunga** kauli hii. (Alama.2)
(b) Taja **bahari kuu** ya ushairi ambayo imetumiwa na mshairi. **Fafanua**. (Alama.2)
(c) Fafanua dhamira ya mshairi. (Alama.2)
(d) Kwa kutoa mifano bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (Alama.2)
(e) Eleza jinsi mshairi ametumia idhini ya ushairi katika utungo huu. (Alama.2)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

(f) Andika ubeti wa nne kwa lugha natharia. (Alama.4)
(g) Mshairi anamaanisha nini anaposema _zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,‘ (Alama.2)
(h) Eleza toni ya shairi hili. (Alama.2)
(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao.
i) Nitatongoa
ii) Zitapusa. (Alama.2)

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 8

KISWAHILI

KARATASI YA 102/1

INSHA.

MUDA: SAA 1¾

1.lazima

1. Siku za hivi karibuni umesoma riwaya mpya iliyoandikwa na Msanifu Kombo inayoitwa : Afrika imelaaniwa. Andika tahakiki ya riwaya hii.

2.Hatua ya serikali kuu kumpa kila mwanafunzi wa darasa la kwanza tarakilishi ni manufaa sana. Jadili

3.Andika kisa kitakachodihirisha ukweli wa methali ifuatayo:

Ukiona cha mwenzako kikinyolewa na chako tia maji

4.Andika insha itakayomalizikia kwa kauli hii: Ama kweli sikufikiria wala kutegemea kuwa aushi yangu ingebadilika jinsi hiyo.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

KCSE PREDICTOR 8

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya pili
Lugha
MUDA:SAA 2 ½
KIDATO CHA NNE

1.UFAHAMU (Alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake mkuu.

Yeye hutarajia kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia watoto na daima dawamu kuwa **'mwendani wa jikoni'** akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. Akanyagapo **mume naye papo huutia wayo wake.**

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, Historia, Jiografia, Hesabu, Sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya. Akataka kuwa mwalimu, akawa.Akataka kuwa daktari, akafanikiwa.Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa **hateswi akafyata ulimi.** Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali 'mahali pake' katika jamii alipotengewa na wanaume wenye **mawazo ya kihafidhina** yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha **ukatani.**

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo, lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanamume wa 'kisasa', ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama mshiriki sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya **aushi.**

Maswali

a) i) Msemo 'mwendani wa jikoni' unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii?(alama1)

……

……

ii) Thibitisha hali uliyotaja hapo juu kwa kutoa hoja nne. (alama 2)

……

……

……

……

b) Mwandishi ana maana gani anaposema 'akanyagapo mume naye papo huutia wayo wake' (alama 1)

……

……

c) Tofautisha mwanamke wa kiasili na wa kisasa ukizingatia maswala ya ndoa na elimu. (alama 4)

……

……

……

……

d) Eleza hoja sita zinazoonyesha kuwa wanaume wana 'mawazo ya kihafidhina' dhidi ya mwanamke. (alama3)

……

……

……

……

……

……

e) Fafanua athari zinazotokana na mabadiliko ya mwanamke wa kisasa katika jamii kulingana na mwandishi. (alama2)

……

……

……

……

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 2)

i. Ukatani

……..

ii. Aushi

……..

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma kifungu kifauatacho kisha ujibu maswali.

Mifuko ni muhimu sana katika maisha ya binadamu ya kila siku. Baadhi ya mifuko huundwa kwa namna ambayo inadumu na inaweza kutumiwa mara kadha wa kadha. Hii huweza kuhifadhiwa na kutumiwa kwa kipindi kirefu. Asilimia kubwa ya mifuko ya aina hii hutengenezwa kutokana na nguo au ngozi. Hata hivyo, ipo mifuko mingine ambayo si ya uashi, haidumu. Hii ni mifuko myepesi, rahisi kubebeka na inayopatikana kwa wingi sana. Hii ni mifuko ya plastiki.

Mifuko ya plastiki hupatikana katika maeneo mengi sana. Mifuko hii sio ghali inapolinganishwa na ile ya nguo au ya ngozi. Hii ni ya gharama ya chni na hupendwa kutokana na wepesi wake. Hata hivyo, mifuko hii inaweza kuwa chanzo cha matatizo mengi. Matatizo haya hutokana na linalopasa kufanywa kuhusu mifuko hii baada ya kutumiwa kwake. Mifuko ya nguo ambayo inatupwa kwenye jalala huishia kuoza na kuwa sehemu ya uchafu wa jalala hilo. Kwa upande wake, mifuko huo. Hata inapofukiwa arthini haiwezi kuoza hata kama kufukiwa huko ni kwa miaka mingi. Aidha hata pale inapochomwa, haiwezi kuteketea hadi kuwa jivu kama ilivyomifuko ya karatasi.

Upo umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa sera madhaubuti za kupambana na tatizo la mifuko hii. lazima zitungwe sheria ambazo zinakabiliana na uchafuzi wa mazingira kwa njia hii. kwa njia hii hatari zianzowakabili watu na wanyama zitapunguzwa kwa kiasi kikubwa. Kwa hakika njia mojawapo ambayo ingeweza kutumiwa ni kuharamisha matumizi ya mifuko hii katika upakiaji. Sheria zinaweza kupitishwa ambazo zinahimiza matumizi ya mifuko mbadala kama ile ya karatasi kubebea vitu vidogo Fauka ya hayo,

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

pana haja ya kuwazia kuwepo kwa njia nzuri kuteketezea mifuko hiyo. Inawezekana kuhimiza watumiaji kuirejesha mifuko hiyo mahali Fulani kwa ajili ya uteketezaji huo. Hata hivyo, hali hii huenda ikawa ngumu kwa kuwa inahitaji nidhamu ya hali ya juu sana kwa upand ewa watumiaji.

(a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 105 – 110. (alama 10, 1 utiririko)

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Nakala safi

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Eleza mawazo makuu yanayojitokeza katika aya ya mwisho (maneno 50 – 55) (alama 5, 1 utiririko)

Matayarisho

……

……

……

……

……

Nakala safi

……

……

……

……

……

……

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA **(Alama 40)**

a) Taja sauti mbili zinazotamkiwa kwenye kaakaa laini (alama 1)

……

b) Eleza tofauti za sentensi zifuatazo (alama 2)

i) Amerudi shuleni!

……

ii) Amerudi shuleni.

……

c) Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mstari.

i) Afisa mkuu anafuata sharia <u>sembuse</u> wewe. (alama 1)

……

……

ii) Ameenda huko mbali <u>sokoni</u> (alama 1)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

……

……

d) Tambua aina ya vihusishi katika sentensi zifuatazo

i) Jumba alifuatalo li mbele ya msikiti wa Musa (alama 1)

……

……

…

ii) Kisiwa cha Ginigi kimekauka (alama 1)

……

……

…

e) Tambua hali katika sentensi ifuatayo.

Vyungu vya aina hii vyafinyangwa na huyu. (alama 1)

……

……

…

f) Toa maana mbili za neno lifuatalo (alama 2)

Somo

……

……

g) Kanusha

Mama alimwambia sipo alime haraka (alama 1)

……Nyambua

vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano

i) Lia (Kutendeshwa) (alama 1)

……

ii) -Ja (Kutendea) (alama 1)

……

h) Andika katika hali ya wastani umoja

Kigombe kile kiliumia kikwato (alama 2)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

……

……

i) Akifisha sentensi ifuatayo.

Je kuna manusura wowote yeye alitaka kujua. (alama 2)

……

……

j)

i) Eleza maana ya kirai (alama 1)

……

……

ii) Onyesha aina ya virai katika sentensi ifuatayo.

Nilimpata akilalama ndani ya darasa (alama 2)

……

……

k) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.

Mwelekezi wake alimwambia kuwa angeweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa angeyafuata mashauri yake. (alama 2)

……

……

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale.

Mtoto mmoja aliyekuwa mgonjwa sana alitibiwa jana. (alama 4)

……

……

……

……

……

……

……

……

m) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia “o” rejeshi

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo (alama 1)

……

……

…

n) Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo

Wachimba migodi wanafanya kazi haraka ipasavyo. (alama 2)

……

……

o) Tumia kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi katika sentensi (alama 2)

……

……

p) Onyesha viambishi katika fungutenzi hili (alama 2)

Sajilika

……

……

…

q) Eleza matumizi ya "na" katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Ndovu aliuawa <u>na</u> wawindaji haramu <u>na</u>mi nikawaripoti

……

……

…

r) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo (alama 2)

i) Takrimu

……

……

ii) Sakini

……

……

s) Weka vitenzi hivi katika hali ya kuamrisha kulingana na maelezo katika mabano(alama 2)

i) -nywa (umoja)

……

……

ii) Tubu (wingi)

……

……

t) Weka neno lifuatalo katika ngeli mwafaka (alama 1)

Nyasi

……

……

4. <u>ISIMU JAMII (ALAMAMA 10)</u>

Eleza sababu za vijana kutumia lugha ya sheng’ (alama 10)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 9

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: Saa 2 ½

SEHEMU A

LAZIMA -RIWAYA

CHOZI LA HERI- A. MATEI

1. "Riwaya ya Chozi la Heri inaakisi uozo uliomo katika Jamii nyingi barani Afrika"

   Thibitisha kauli hii kwa kurenjerea Riwaya (al 20)

SEHEMU B

TAMTHILIA KIGOGO (P. KEA)

2. "Do ! Do ! Simameni ! Simameni! leo kutanyesha mawe ! "

   i. Eleza muktadha wa dondoo hili (al 4)

   ii. Fafanua mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili (al 4)

   iii. Huku ukitoa mifano jadili hoja sita zinazodhihirisha jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika Tamthilia ya kigogo (al 12)

AU

3. Kwa kuirejerea Tamthilia ya Kigogo eleza jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya Majazi (al 20)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

SEHEMU C

HADITHI FUPI

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

(A.Chokoko na D.Kayanda)

4. "Kwetu tunapigania mikono ielekee vinywani. Mzoea vya sahani, vya vigae haviwezii"
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili
      (al 4)
   b) Tambua tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili
      (al 2)
   c) Fafanua sifa nne za msemaji
      (al 4)
   d) Jadili maudhui ya utabaka ukirejerea hadithi husika
      (al 10)

AU

5. Jadili maudhui ya usaliti katika hadithi;
   a) Mapenzi ya kifaraurongo
      (al 10)
   b) Mame Bakari
      (al 10)

SEHEMU YA D

USHAIRI

6. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali.

Mungu naomba subira, subira nayo imani

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Imani iliyo bora, bora hapa duniani
Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani
Hiani pamwe ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhulu
Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri wangu muwili
Muwili hata kidari, kidari kuwa thakili
Thakili kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele
Muwele wa hitilafu, hitilafi ya nduwele
Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele
Milele kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vitomele vikwato
Vikwato pia maole, maole kufanya mito
Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto
Kitoto kilo vipele, vipele vyenye fiakuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka
Kutamka wazi vino, vino subira kutaka
Kutaka imani mno, mno n'sipate wahaka
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.

Mashaka haya ya leo, leo yawe yarnepita
Yaniepita na vilio, vilia vipishe nyota
Nyota njema ingarao, ing'arao kunikita
Kunikita salamani, salamani nikadata.

a) Kwa nini nafsi neni inaomba subira na amani ? (alama 2)

b) Shairi hili ni la Bahari gani kwa kuzingatia : (alama 4)

i) Mpangilio wa maneno

ii) Mpangilio wa vina

c) Kwa kutokea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (alama 4)

d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)

e) Kwa kutolea mifano, eleza jinzi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa kutekeleza arudhi. (alama 6)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

AU

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali. (alama 20)

Barabara.

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili
Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
Kuwa tayari kupanda na kushuka.‖

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka.

Jambo moja nakumbuka: Mungu

Je, nimwombe tena? Hadi lini?

Labda amechoshwa na ombaomba zangu

Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini

Lazima niendelee kujitahidi kwa kila hatua mpya

Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu

Nikinaswa na kujinasua

Yumkini nitafika mwisho wake

Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.

(Timothy Arege)

Maswali.

(a) Taja na ueleze aina ya shairi hili.
(alama 2)

(b) Eleza toni ya shairi hili.
(alama 2)

(c) Fafanua dhamira ya shairi hili.
(alama 2)

(d) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili.
(alama 3)
(i) Tanakali za sauti
(ii) Mbinu rejeshi
(iii) Taswira

(e) Eleza umhimu wa maswali balagha katika shairi.
(alama 2)

(f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari.
(alama 4)

(g) Eleza matumizi ya mistari mishata katika shairi hili.
(alama 2)

(h) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi.
(alama 3)
(i) Kuruba
(ii) Siha
(iii) Machweo

SEHEMU E FASIHI SIMULIZI

8. Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yaliyoulizwa.

Hapo zamani za kale, Mungu alituma wajumbe wawili waende duniani. Wajumbe hawa ni Kinyonga na Mjusi. Kwanza alimtuma Kinyonga na kumwagiza akaseme "wanadamu hamtakufa." Kinyonga alienda kwa mwendo wa kuduwaa, akasimama hapa na pale akila matunda ya miti. Kwa sababu ya hali hii alichelewa sana kufikisha ujumbe kwa binadamu.

Baada ya muda kupita, Mungu alimtuma Mjusi na ujumbe akaseme, "Mwanadamu sharti kufa." Mjusi aliunyanyua mkia akafyatuka pu! Mbio akawahi duniani kabla ya kinyonga kuwasili. Kwa haraka alitangaza agizo kuu, "Wanadamu sharti kufa!" Akarejelea haraka kwa Mungu. Baada ya muda kinyonga naye akafika duniana na kutangaza, "Wanadamu hamtakufa!" Wanadamu wakapinga mara na kusema, "La! Tumeshapata ujumbe wa Mjusi, wanadamu sharti kufa! Hatuwezi kupokea tena neno lako! Basi kulingana na neno la mjusi, wanadamu hufa.

a) . Tambua aina hii ya hadithi (al 2)

ii. Toa sababu za jibu lako katika (a) i. (al 1)

b) Eleza sifa tatu zinazohusishwa na ngano za fasihi simulizi katika hadithi hii. (al 3)

c) Fafanua hulka mbili za Kinyonga kwa mujibu wa makala haya (al 2)

d) Hadithi hii ina umuhimu gani? (al 4)

e) Taja njia zozote nne za kukusanya kazi za fasihi simulizi (al 4)

f) Fafanua jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi (al 4)

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 9

KISWAHILI

PAPER 1

Swali la kwanza ni la lazima

1. Wewe n imtaalamu wa masuala ya haki zawatoto. Andika mahojianobainayakonamwanahabarikuhusukutekelezwakwa motto wakiumekatikajamii

2. JadilinafasiyaushaurinasalakatikashulezaUpiliilikudumishanidhani

3. Andikakisakitakachodhirihishamaanayamethalihii. Mwenyekovuusidhanikapoa

4. Tungakisakinachoanzanamanenoyafuatayo.
Nilijaribukuuinuamguuwanguuliojaamaumivukutokananajeraha.

KCSE PREDICTOR 9

102/2 LUGHA
1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

HISTORIA YA KATIBA

Katiba ni utaratibu wa sheria unaoweka mpango wa jamii kuendesha mambo. Ni muhimu kila raia ajue katiba ya nchi yake.

Katiba yaweza kuwa imeandikwa au haikuandikwa. Katika jamii za jadi katiba ilihifadhiwa na kupokezwa kwa mdomo. Mwindo wa kuandika katiba ulianza nchini Marekani mwaka 1787. Ingawa katiba hii imefanyiwa mabadiliko hapa na pale,bado ni ileile. Kenya ilipowekwa chini ya himaya ya Uingereza mwaka 1895, ilianza kutumia katiba ya Uingereza. Baada ya masetla wa kikoloni kujikita, Kenya kuwa koloni. Hii ililazimu pawe na katiba nyingine mwaka 1920. Waafrika waliupinga mfumo huu kwa sababu haukuwahusisha kikamilifu kwenye masuala ya uongozi. Utetezi wa wanasiasa uliilazimisha serikali ya Uingereza kuitisha makongamano mbalimbali kama vile lile la Devonshire na mengine ili kurekebisha katiba. Waafrika hawakuridhika. Wakaendelea kudai katiba mwafaka. Harakati hizi zilileta kuitishwa kwa kongamano la katiba la Lancaster. Lengo lilikuwa kuandika katiba itakayotumiwa nchini hadi leo. Kati ya wajumbe walioenda Uingereza kuandika katiba mwaka 1962 ni pamoja na Tom Mboya, Jean Marie Seroney Julius Kiano, Jomo Kenyatta, Masinde Muliro, Oginga Odinga, Ronald Ngala Daniel Arap Moi na James Gichuru. Wengine ni Martin Shikuku, Dennis Akumu, Taita Towett, Abdilahi Nassir, Jeremiah Nyaga na John Keen.

Katiba ni kitovu cha taifa. Baina ya mambo inayotekeleza ni kuweka utaratibu na kanuni za utawala, kwa mfano, utawala wa kimikoa na serikali za wilaya. Pamoja na haya, katiba hufafanua vyombo vikuu vya serikali ,mamlaka yavyo na mipaka yavyo ya kutenda. Vyombo hivi ni bunge, mahakama, urais, jeshi n.k. Hali kadhalika, katiba hupambanua haki za raia.

Hii hudumisha demokrasia na huwawezesha wananchi kupata uhuru na haki za kimsingi. Katiba hukinga haki za kila raia, hasa kutokana na udhalimu wa wengi au wenye uwezo mkubwa. Zaidi ya yote, katiba huimarisha asasi za umma ili kudumisha uwajibikaji.

Katiba huhalalishwa na watawaliwa. Hii hutokea wanaposhirikishwa katika uandishi wake. Kuanzia miaka ya themanini, raia walianza kudai katiba igeuzwe. Mwamko wa kutaka mageuzi ulianza kwa harakati za kubadilisha mfumo wa kisiasa kutoka ule wa chama kimoja hadi ule wa demokrasia ya vyama vingi. Haja ya mfumo mpya wa kisiasa ulilenga kuwashirikisha wananchi katika utawala na kuondoa uimla.

57

Harakati zilitia fora miaka ya tisini. Mambo yaliyochochea hali hii ni mengi. Kwanza, katiba iliyokuwa imeandikwa na watu wachache ilikuwa imefanyiwa marekebisho mengi. Marekebisho haya yalimpa rais mamlaka mengi juu ya serikali kuu na vyombo tofauti vya serikali. Pili, viongozi na watu wenye uwezo na utajiri walipuuza katiba. Raia walihisi wanadhulumiwa. Walipinga hali ya wachache waliomzunguka rais kunufaika huku umma ukitengwa. Tatu, kutokana na uongozi uliokuweko wakati huo, wanawake, watoto na walemavu walidhulumiwa na kukosa uwakilishi ufaao.Hatimaye, pakawa na ongezeko la uharibifu wa mazingira, ufisadi na unyakuzi wa mali ya umma kama vile ardhi.

Waliopigania katiba mpya walikuwa na haja ya katiba ambayo uandikaji wake ungewahusisha Wakenya wote. Mwanzoni, serikali ilipinga wito wa mabadiliko. Lakini mnamo mwaka 2001 iliunda Tume ya Marekebisho ya Katiba ili kutekeleza mahitaji ya wananchi. Tume hii iliwahamasisha na kuwashawishi raia kutoa maoni. Tume iliandaa vikao katika maeneo ya ubunge 210 ambapo wananchi walitoa mapendekezo kuhusu marekebisho ya katiba waliyotaka.

Katika mapendekezo hayo raia walisisitiza mambo kadhaa. Jambo la kwanza ni utawala mwema na uwajibikaji wa viongozi na maafisa wa umma .Jambo lingine ni kulinda haki za binadamu zikiwemo za wanawake, watoto na walemavu. Raia walidai kanuni za usawa na ulinganifu. Aidha walitilia mkazo mahitaji ya msingi kama chakula, afya nzuri, makao, elimu, usalama, uchumi, na kadhalika.

Msingi wa mapendekezo hayo yote ni kuwepo na amani ya kitaifa, umoja na uadilifu ili kulinda maslahi ya wananchi wote na taifa.

Maswali :

a) Eleza kilichosababisha kongamano la katibala Lancaster. (3mks)

- ---

- ---

- ---

- ---

-

b) Taja mambo matatu yaliyotiliwa mkazo na raia katika maoni yao kuhusu katiba. (alama 3)

- ---

- ---

- ---

-

---

c) Eleza umuhimu wa katiba kwamujibu wa taarifa. (alama 3)

- ---
- ---
- ---
- ---

d) Taja sababu zilizochangia ubadilishaji wa katiba. (alama 3)

- ---
- ---
- ---
- ---

e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)
i) Kitovu

- ---

- ---

ii) Harakati

- ---

- ---

iii) Hamasisha.

- ---

- ---

2. **UFUPISHO. (ALAMA 15)**

Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata.

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana.Akiwa na nidhamu hiyo, atakuwa mtu mwadilifu, anayeweza kustahiwa na kusadikika katika mambo, shughuli na hali tofauti

Kwanza, mtoto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani mwao, shuleni na pia katika jamii.Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa vijulanga wote wanamtegemea kama msimamizi wa mambo nyeti ya maisha yao. Kwa hivyo, ni dhahiri shahiri kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume na mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili, huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, mathalani jukumu ama dhima fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Watu hapana shaka watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambao tayari wamekwisha tiliwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadalifu daima atajiepusha na shutuma na majanga yote yanayoweza kuchipuka. Kuna msemo maarufu, kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu kwamba "aliye kando haangukiwi na mti."Pia waliambiwa kwamba, " pilipili usiyoila yakuwashiani?"

Ni bayana kutokana na misemo hiyo miwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuwakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya 'watoro' ambao ni utovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozo na mielekeo ya watu wazima ambao wako mazingirani mwake.Ndipo wakale wale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbani hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kufikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu wote katika maisha yake.Ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayana kwamba mabaya yote ayatendayo duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani,watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu. Ni kheri mja kujitahidi mwenyewe, kwani uhalifu haulipi chochote.

a) Nini umuhimu wa nidhamu? (maneno kati ya 50-55) (al. 1 ya mtiririko)
(alama 7)

Matarisho.

--

Jibu

-

---

b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (tumia maneno 55-60)
(mtiririko alama 1) (alama 8)

--Jibu

---

3. MATUMIZI YA LUGHA.

a) Onyesha muundo wa silabi ya kwanza katika maneno yafuatayo. (alama 2)

i) Chura

--

ii) Mbali

--

b) Taja vigezo vya kuainisha irabu. (alama 2)

----

c) Taja majukumu mawili ya viambishi awali katika kitenzi. (alama 2)

--

d) Andika ukubwa wingi wa sentensi ifuatayo.

Mbuzi yule ameumia mguu. (alama 2)

--

-

e) Eleza ni kwa nini neno samehe ni la asili ya kigeni. (alama 1)

--

f)Sahihisha sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mwanafunzi mwenye aliimba funguo yangu amepatikana.

--

g) Eleza matumizi ya kiambishi ‘ku’ katika neno lifuatalo. (alama 1)

hakukunyesha.

--

h) Onyesha mzizi na viambishi katika neno lifuatalo. (alama 2)
Wafao.

--

-

i) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama 2)
“Fika mapema nikutume sokoni,” mama alimwambia mwanawe.

--

j) Bainsisha virai katika sentensi ifuatayo .
Anachukia kusoma riwaya yenye masuala ya kisiasa. (alama 3)

--

---

k) Yakinisha katika nafsi ya tatu wingi. (alama 2)

Sijasafiri kwenda marekani.

-

--l) Changanua sentensi ifuatayo kwa mchoro wa matawi.

Mjomba anamkama ngombe wake. (alama 3)

-

--

---

m) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi ya shamirisho zifuatazo. (alama 3)
i) Kutondo
ii) Kipozi
iii) ala

--

-

n) Andika kinyume cha sentensi hii. (alama 2)
Watoto wameombwa waanike nguo.

--

o)Tumia kiambishi ‘ndi’ katika sentensi kama kishirikishi. (alama 1)

--

p) Tofautisha sentensi zifuatazo kimaana. (alama 2)
i) Tulipofika hotelini tulipewa soda na chupa.
ii) Tulipofika hotelini tulipewa soda kwa chupa.

--

q) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi ya alama zifuatazo. (alama 2)
i) Kibainishi
ii) Parandesi

--

r) Bainisha ngeli za maneno yafuatayo. (alama 2)
i) Uhondo

--

ii) Pua.

--

s) Tumia neno hadi kama kihusishi cha (alama 2)
i) Wakati

--

ii) Mahali.

--

t) Andika sentesi ifuatayo upya kulingana na maagizo.(alama 2)
Mkoba wa babu una viroboto (Anza kwa viroboto)

--

4. **ISIMU JAMII**

I) " Beba! Beba-aa! Kila stage ni bao, kumi haitoshi hata adazi . Funga mshijpi karau mbele. …….

a) Tambua sajili hii (alama 2)

--

b) Eleza sifa nne zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 4)

-

---

c) Fafanua mambo manne yanayotatiza maendeleo ya Kiswahili shuleni. (alama 4)

--

--

--

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 9

K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI

1. lazima

(a) Miviga ni nini? (alama2)

(b) Eleza sifa **tano** za Miviga (alama 5)

(c) Fafanua hasara **tatu** za miviga (alama 3)

(d) Eleza changamoto **tano** ambazo mtafiti hukabiliana nazo anpokusanya data ya miviga

(alama 10)

SEHEMU B:
TAMTHLIA – Kigogo (Pauline Kea)

2. Onyesha namna mwandishi alivyofanikiwa kukuza maudhui yafuatayo

(i) Elimu (alama 10)
(ii) Ujana (alama 10)

2. Mvunja nchi ni mwananchi ‘Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea matukio katika tamthlia ya kigogo (alama 20)

SEHEMU YA C: USHAIRI

B. Moyo wanambia imba,dikteta simwimbie
Moyo wanambia lumba,muhitaji mlumbie
Moyo wanambia chimba,maovu uyachimbue
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia kuwa,ila kasuku usiwe
Moyo wanambia iwa,kunguni ila usiwe
Moyo wanambia pewa,cha mnyonge usipewe
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Moyo wanambia nenda,penye dhuluma senende
Moyo aanambia penda,mnyonyaji simpende
Moyo wanambia ponda,ateswaye simponde
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia tenda,lenye jamala litende
Moyo wanambia unda,lenye faida liunde
Moyo wanambia tunda,lisilo sumu litunde
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia ota,kuwa mwizi usiote
Moyo wanambia kata,marija yote ikate
Moyo wanambia teta,penye dhuluma patete
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nyosha,penye na kombo panyoshe
Moyo wanambia usha,mateso yote yaushe
Moyo wanambia isha,yenye majonzi yaishe
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia waza,yalopita yawazie
Moyo wanambia kaza,mwovu njia mkazie
Moyo wanambia vuaza,lenye heri tuvyazie
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

(Shairi la mbegu la E. Kezilahabi, 1988)

(a) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)

(b) Ainisha bahari za ushauri huu kwa kutegemea
(i) Mpangilio wa maneno
(ii) Vipande vya mishororo
(iii) Idadi ya mishororo kwa kila ubeti (alama3)

(c) Tambua aina **moja** ya urudiaji na utolee mfano (alama 2)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

(d) changua muundo wa shairi hili (alama 4)

(e) Andika ubeti wa **tano** kwa lugha ya nathari (alama 4)

(f) Onyesha aina **moja** ya uhuru wa kishairi aliotumia mwandishi katika shairi lake (alama 2)

(g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika ushairi (alama 2)
(i) Dikteka
(ii) Kasuku
(iii) Mnyonyaji

USHAIRI

Ni mimi nizamishaye chini Mizizi kwenye
majabali Kufyonza chumvi!

Ni mimi ninyunyizae maji

Ili mimea ifumbue

Nafasi zao hewani

Ili miti ishike mimba kuzaa

Matunda,nafaka,mizizi na viazi Ela mimi sili
hata punje moja Nabaki mtupu!

Ni mimi tumbo kubwa,

Niliyeshiba madini

Ni mimi ninayechimba

Kupakua raslimali

Dhahabu,chuma,makaa… ela yote
yanaona Yatiririka kwao!

Nabaki mtupu!

Vyakula vyote nazalisha mimi Na mi'
nabaki na njaa!

Nguo zote nawapa mimi Na
mi'nabaki u tupu!

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Madini yote nawapa mimi

Na mi'nabaki kununua vyao!

Kazi zote nafanya mimi Wao wabaki
kunila nguvu!

Wao wanajita bora

Na mi' nabaki fukara!

(Shairi la S.A Mohamed Jicho la ndani, Longhorn Publishers 2002)

(a) Lipatie shairi hili anwani mwafaka (alama 2)

(b) Fafanua aina moja ya taswira katika shairi hili (alama 2)

(c) Eleza ujumbe mkuu wa mtunzi wa shairi hili (alama 2)

(d) Huu ni ushairi wa aina gani.Toa sababu ya jibu lako (alama 2)

(e) Eleza toni ya ushairi (alama 2)

(f) Mtunzi ametumia mbinu zipi kukuza ujumbe wake (alama 4)

(g) Huku ukitolea mifano onyesha matumizi ya mistari mishata katika shairi hili (alama 2)

(h) Onyesha umuhimu wa kinaya katika shairi hili (alama 2)

(i) Tambua nafsineni katika shairi hili (alama 2)

SEHEMU D:

Hadithi fupi (Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine)

6 Onyesha namna nafasi ya mwanamke inavyosawiriwa kwa kuzingatia hadithi zifuatazo

(a) Ndoto ya Mashaka
(b) Masharti ya Kisasa
(c) Mapenzi ya Kifaurongo
(d) Shogake Dada ana Ndevu

7 . ….Ati umebakwa!Nani akubake wewe? Wapi utakapobakwa mji pasiwe na mtu wa kukuombea?

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Eleza sifa mbili na umuhimu wa msemaji wa maneno haya (alama 4) (c) Jadili maudhui makuu katika dondoo hili (alama 12 (6 x 2)

SEHEMU YA E:

Chozi la Heri (alama 20)

8. Jadili ufaafu wa anwani ***Chozi la Heri.***

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 10

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

SAA:1 ¾

1. **Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Zindukeni ukitoa maoni kuhusu sekta ya usafiri wa pikipiki.**

2. **Fafanua njia mbalimbali za kustawisha michezo nchini.**

3. **Andika insha inayoafikia methali, Ukiona vyaelea vimeundwa.**

4. **Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:**

   Nilijaribu kuuinua mguu wangu uliojaa maumivu kutokana na jeraha…..

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

KCSE PREDICTOR 10

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

SAA: $2^{1}/_{2}$

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia

Kitengo cha familia Kimesakamwa na wimbi kali la mabadiliko katika jamii. Namna ambavyo familia zinaendeshwa siku hizi ni tofauti na taratibu za azali. Waama hakuna kipenge cha maisha yetu ambacho hakijaathiriwa na kile ambacho kimekuja kujulikana kama 'usasa'.

Familia nyingi hasa katika maeneo ya mijini zinategemea sana watu wa kuajiri kuzishughulikia. Wazazi wengi hawatengi muda wa kukaa nyumbani na watoto ili kuwapa mwongozo na mapenzi yaliyo muhimu katika hatua mbalimbali za ukuaji wao. Wazazi huondoka mapema sana kwenda kazini na kurejea wakiwa wamechelewa mno. Watoto wao wakati huo huwa ama hawajaamka au tayari washalala. Kwa upande mwingine wapo wazazi ambao wanafanya kazi katika miji iliyo mbali na wanapokaa watoto wao au nchi za kigeni. Uhusiano kati ya mzazi na mtoto unakosa rotuba ya kuuneemesha na matokeo yake huwa ni vijana waliokosa mwelekeo. Walivyosema Waswahili, samaki hukunjwa akiwa bado mbichi. Tabia za watoto hawa zinaweza tu kuandaliwa katika maadili wakiwa wadogo.

Tofauti kati ya wazazi, Pamoja na kuzaliwa kwa watoto nje ya ndoa kumebadilisha sura ya kitengo cha familia. Tofauti na zamani, hii leo utapata familia ambazo zinaendeshwa na mzazi mmoja – anaweza kuwa baba au mama tu. Ni kweli kwamba mtoto huhitaji malezi ya wazazi wote wawili. Mwongozo wa ushirikiano wa wazazi wote wawili ni imara na bora zaidi kuliko wa mzazi mmoja. Hii haimaanishi kuwa mtoto hawezi kulelewa vizuri na mzazi mmoja au vibaya na wazazi wote. Mtoto huweza kukosa huduma za kimsingi kwa kosa lisilo lake.

Jukumu la jamii katika malezi ya watoto limepungua. Zamani malezi ya mtoto yalikuwa jukumu la kila mwanajamii. Mtoto alipothubutu kufanya kosa aliweza kuadhibiwa palepale na mwanajamii yeyote ambaye hakusita kujitwika jukumu la mzazi. Hata hivyo hali ni tofauti hii leo.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Kumwadhibu mtoto wa mtu ni kichocheo tosha cha kuleta mfarakano usiokwisha katika jamii. Kila mtu anauchelea ugomvi wa kujitakia. Kila mtoto sasa anaelewa na vipimo vya mzazi wake na siyo vya jamii pana. Watoto nao wamegundua hili na hawakusita kujivika mavazi mawili tofauti, zuri mbele ya wazazi wao na jinginelo popote pasipo hao wazazi. Sasa wazazi wanaweza kuishi na wahalifu waliokubuhu bila kufahamu.

Jambo lingine linalohusiana na hilo ni kutupiliwa mbali kwa tamaduni za Kiafrika. Ni kama jamii iliyotupa jongoo na mti wake. Si siri kuwa kuna masuala ya kitamaduni yaliyopitwa na wakati na ambayo inahalisi kuyapiga teke. Hata hivyo hatuwezi kukitia kila kipengee cha tamaduni zetu jalalani. Utamaduni wetu mbali na kututambulisha kama jamii, pia hutekeleza jukumu adhimu la kutuwezesha kuyaona mambo kwa mtazamo mmoja. Mtazamo huo mmoja ndio unaotupa umoja wetu. Hatuwezi kuwa na utangamano bila kuwa na uzi unaotufunga Pamoja. Maadili ya jamii hayawezi kubainika bila ya watu kuwa na Mwongozo na mtazamo mmoja kuhusu hali yao ya maisha.

Familia za kisasa zina idadi ndogo za watu ikilinganishwa na hapo awali. Hali ngumu ya maisha imewasukuma watu katika kupata watoto wachache ambao wanaweza kumudu kuwalea vizuri. Nako kupungua kwa nafasi za ajira kunawazuia vijana kuingia katika nikahi mapema. Hali hii imechangia katika kupunguza idadi ya watu na pia kupunguza kasi za uchipukaji wa familia mpya. Hali ngumu ya maisha imepunguza upana wa familia kama ilivyokuwa awali. Siku hizi mtu na mkewe au mumewe Pamoja na watoto wanaikamilisha familia. Vikoa vimekwisha na kubaki kuwa kila mtu na lake. Wengine hawako tayari kuwatilia pondo ndugu zao.

Maswali

1. Kwa mujibu wa taarifa eleza matatizo yanayoweza kuikabili familia inayoendeleshwa na mzazi mmoja. (alama 2)

   .....

   .....

   .....

2. Ni nini kiini cha utengano wa wazazi katika ndoa. (alama 1)

   .....

   .....

3. Jadili nafasi ya utamaduni katika kuijenga jamii bora kwa kurejelea makala. (alama 2)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

.....

.....

.....

4. Kwa nini familia za kisasa zina idadi ndogo ya watu? (alama 2)

.....

.....

.....

.....

5. Taja huku ukitoa mifano ya tamathali zozote tatu za lugha zilizotumiwa katika taarifa. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

.....

6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kifunguni. (alama 5)

   i. Kimesakamwa –

   .....

   .....

   ii. Mfarakano usiokwisha

   .....

   .....

   iii. Wahalifu waliokubuhu

   .....

   .....

   iv. Vikoa vimekwisha

   .....

   .....

   v. Kujivika mavazi mawili

.....

.....

2. **UFUPISHO**

Soma ***taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo***

Ki1a walimwengu wanapotajiwa kuwa shambulizi la kigaidi limetokea mahali fulani, wimbi la taharuki huwakumba. Mashambulizi ya kigaidi yameongezeka katika siku za hivi majuzi ambapo kundi Ia watu linalohisi kuwa linaonewa na kukandamizwa huitumia mbinu ya kushambulia kwa kuvizia, hasa kutumia mabomu au kuteka ndege na kutishia kuilipua na wakati mwingine kuilipulia angani. Kuna mabomu yaliyotegwa na kulipuka katika maegesho ya magari au kwenye vizuizi vya magari. Mengine hutegwa na kulipuliwa katika afisi, mikahawa, makao ya watu, n.k. Katika baadhi ya mashambulizi, wapo waliojitoa mhanga ambao hujilipua katika shambulizi

.

Makundi ya watu wanaohasimiana ndio chanzo cha matendo ya kigaidi. Kundi linalohisi kuwa linaonewa au ambalo kweli linaonewa na ambalo ni dhaifu kuliko lile jingine, hufanya juu chini kushambulia kisirisiri. Nia ni kulipisha kisasi kwa jambo wanalohisi wamehiniwa. Kwa kuwa kundi hilo hudhani kuwa dhaifu halina njia wala uwezo wa kuyakabili moja kwa moja matendo waliyotendewa au wanayoendelea kutendewa, njia ya pekee, kwa maoni yao, huwa hii ya kushambulia kwa kushitukiza. Kiini cha uonevu kinaweza kuwa dini, uchumi, maamuzi ya kisiasa au jambo lingine lolote lile. Kinachobainika katika suala zima Ia mashambulizi ya kigaidi ni kuwa lipo jambo ambalo linazikera nyoyo za kundi fulani Ia watu walio wanyonge ambao huona kuwa njia ya pekee ya kudhihirisha hisia zao ni kupitia mashambulizi ya aina hii.

Mashambulizi ya aina hii yana athari zake nyingi. Kuna watu wanaouawa na wengine wengi kulemaa. Maisha ya watu hawa au jamaa zao wanaowategemea hubadilika na kujaa mvurugano uliokithiri. Kuna watoto ambao ndoto zao za kupata elimu zimetumbukia nyongo baada ya wazazi wao kuzikwa hai katika vifusi. Mbali na kukosa elimu na mahitaji mengine ya kimsingi, watoto hawa hupatwa na matatizo ya kisaikolojia baada ya kuona maafa yaliyowafika wavyele wao. Hata wale wanaosalimika kutoka kwenye vifusi hivi hawaishi kuandamwa na majinamizi yasiyoisha.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Mashambulizi ya kigaidi hayaathiri tu watu pamoja na kuharibu mali ya thamani ya lukuki ya pesa. Zipo athari nyingine hasi ambazo hudhihiri. Kwa mfano usalama wa nchi huwa mashakani. Wananchi na wageni vilevile hujihisi kuwa dhaifu na dhalili katika nchi illyovamiwa. Serikali husika hujikuta katika shutuma kwa kushindwa kutambua mipango hiyo mapema na kuzuia hasara ya nyoyo na mali. Aidha, jamii ya kimataifa huiona nchi hiyo kama yenye kukosa usalama na hivyo kuwaonya raia wake dhidi ya kuizuru. Iwapo nchi husika inategemea utalii kama kitega uchumi muhimu, basi hukosa wateja na waajiriwa katika sekta hii kupigwa kalamu.

Tatizo la ugaidi si Ia nchi moja au mataifa fulani mahususi wala hakuna nchi au taifa linaloweza kudai kuwa haliwezi kukabiliwa na tishio la kigaidi. Kuanzia Dar es Salaam, Nairobi hadi New York na London au hata Cairo hadi Riyadh na Baghdad, sote tunakabiliwa na tatizo hili hili. Hakuna ajuaye lini, vipi au wapi magaidi wamedhamiria kutekeleza unyama huu.

Labda swali Ia kujiuliza ni kwamba; Je, upo uwezekano wa mwenendo huu wa kuwaangamiza watu, wengi wa wahasiriwa wakiwa wale wasio na hatia, kudhibitiwa na kumalizwa kabisa? Serikali za nchi mbalimbali zimejaribu kutumia uwezo wao wa kiuchumi na kiteknolojia ili kujaribu kuiondoa hali hii. Njia waliyoitumia ni ya mtutu wa bunduki ambapo makombora mazito yaliyogharimu pesa nyingi yanadondoshwa katika makao ya washukiwa. Hata katika hatua hii nayo, upo uwezekano mkubwa wa kuuawa watu wasio na hatia vilevile. Pia ni wazi kwamba uhasama unalipwa kwa uhasama na matokeo yake ni ulipizaji kisasi usioisha. Amani inakuwa nadra.
Juhudi za ulimwengu kulaani vitendo hivi ni nzuri ila hazitoshi. Utumiaji nguvu kutafuta ufumbuzi wa kitendawili hiki si suluhisho. Kama wanavyoeleza wanasosholojia, kila kitendo kina sababu zake zilizofichama. Sababu hizo ndizo kichocheo cha vitendo vinavyojidhihiri. Hivyo basi jukumu lipo katika kutambua vichochezi vya mashambulizi na kujitahidi kuvitatua kwa njia ya mashauriano yaliyojengwa katika nia safi ya kuleta usawa na usalama duniani.

Wapo watu wanaoona kuwa vitendo vya mataifa yaliyoendelea kwa nchi changa ndivyo kilele cha ugaidi. Watu wanaona kuwa tabia ya mataifa hayo yenye uwezo kiuchumi na kiteknolojia kuamua na kudhibiti sera na imani za nchi changa ni ugaidi uliokubuhu. Vikwazo hivi huwaacha viongozi hoi na

wananchi kuteseka kufuatia ulazimishaji wa sera za kiuchumi na kisiasa zisizohusiana na mahitaji ya watu wa nchi husika wala kuambatana na mahjtajj ya nchi hizi. Hii ni hali inayoyatia mataifa yanayoendelea katika wasiwasi usioisha kutokana na dhiki zisizoisha kusababishwa na mataifa ya kigeni.

I. UFUPISHO

a) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 80, fupisha aya ya pili, tatu na nne. (alama 10)

alama1, mtiririko

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

b) Eleza njia zinazotumiwa na mataifa ulimwenguni kupambana na ugaidi. (Maneno 40) alama 5; 1 ya mtiririko

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) i.Taja vigezo viwili vya kuanisha irabu. (alama 1)

.....

.....

.....

ii. Tofautisha sauti zifuatazo.(alama.2)

a. /a/ na /i/

.....

b. /e/ na /o/

.....

(b) Ainisha aina za vivumishi katika sentensi ifuatayo.(alama. 2)

Mwalimu mzee alitufundisha vizuri ile mada ngumu.

.....

.....

i. i.Eleza maana ya kirai. (alama.1)

……

……

……..

ii. Tunga sentensi iliyo na kirai kivumishi na kirai nomino chenye muundo wa W+ V (alama 1)

……

……

(c) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia “O” rejeshi. (alama 2)

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

……

……

……..

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

(d) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya udogo wingi.

Kono lake lilivimba baada ya kuumwa na jibwa. (alama 2)

.....

.....

.....

(e) Tunga sentensi iliyo: (alama 3)

Kitenzi kishirikishi kikamilifu

.....

.....

Kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi

.....

Kiwakilishi cha nafsi ya tatu tegemezi wingi.

.....

.....

(f) Kanusha sentensi ifuatayo kisha ueleze maana yake katika hali kanushi (alama 2)

Angeongoza darasa lake, angepewa tuzo.

.....

.....

.....

.....

(g) Onyesha sehemu za kisarufi katika neno lifuatalo. (alama 2)

Kililiwa

.....

.....

.....

(h) Kanusha katika hali timilifu wakati uliopita.

Kamati ya uchaguzi iliandaa ripoti kuhusu utovu wa nidhamu shuleni. (alama 2)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

.....

.....

.....

(i) Changanua kwa kutumia mchoro wa matawi

Hatukuondoka na yeye japo tulirudi naye. (alama 4)

(j) Tumia kiambishi KA katika sentensi ili kuleta dhana ya: (alama 2)

i. Wakati usiodhihirika

.....

.....

ii. Kuonyesha matokeo yanayosababishwa na kitendo.

.....

.....

(k) Chane kwa mtama_____ kwa udongo. (alama 1)

(l) a. Eleza maana ya fungu tenzi. (alama 1)

.....

.....b.Taja aina mbili za fungu tenzi. (alama.2)

.....

.....

(m) Geuza sentensi hii hadi usemi halisi.

Wanakijiji walikuwa wanataka kujua iwapo vipakatalishi vya shule za msingi vingeweza kuinua kiwango cha elimu. (alama 3)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

.....

.....

.....

(n) a. Eleza maana ya yambwa. (alama 1)

.....

.....

.....b. Tunga sentensi iliyo na: shamirisho kipozi na chagizo cha kiasi kamili. (alama.2)

.....

.....

(o) Tunga sentensi kwa kutumia kiunganishi cha wakati.(alama 2)

.....

.....

.....

(p) Andika visawe vya maneno yaliyopigigwa mstari . (alama 2)

Tulienda <u>kusali</u> siku ya <u>Jumapili.</u>

.....

SWALI LA 4: ISIMU JAMII

Eleza changamoto zinazokumba ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 10)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

mwalimuepublishers@gmail.com

KCSE PREDICTOR 10

K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

1. LAZIMA: RIWAYA: CHOZI LA HERI NaAssumptaMatei ALAMA 20

"…Nimeonja shubiri ya kuwa mtegemezi kihali na mali.lakini katika yote hayo, nimejifunza mengi…"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Bainisha tamthilia ya usemii nayo jitokezaka katika kauli hii. (alama 2)
c) Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kumrejelea mzungumzaji.

(ala 14)

2. USHAIRI

ALAMA 20

Soma mashairi haya kasha ujibu maswali yanayo fuata

SHAIRI A

Wewe,
Utazame mlolongo wa
Wajaunaoshikanjialikiwapo;
Unaofuatapembe za barabarazisokuwapo,
mwenyeakili, inampikunayeye;
Kwendakuisakaauni,
Kuitafutakaziinayowalachenga.
Dunia nayakehali, hupumbazahatimaye;
Itazamemigongoyawachapakazi,
Watokwaonajashokapakapana,
Wanaotafunwauhainajualiso huruma:

Wakiinuavyumanamagunia,

Wakiinuamakontena,
Wakichubukamashambani,
Wakiumiaviwandani,
Wakitesekamakazini,
Halafu

Uangalieuleujirawakijungumeko,

SHAIRI B

Dunia kitendawili, hakuna ateguaye;
Dunia kamatapeli, hadaanyingiujuye;
Dunia

Dunia inamizungu, tenayapikamajungu.

Dunia inaakili, binadamusichezeye;
Dunia uwenamali, huiwezidhorubaye;
Dunia inamizungu,tenayapikamajungu.

Dunia wenyemuali, ambaowaichezeye;
Dunia kipigo kali, huwakumbahatimaye;
Dunia wakajakuli, "menipataninimiye?"
Dunia inamizungu, tenayapikamajungu.

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

Mshaharausokifuhaja,

Nguozisizositirimiilidhaifu,

Kilo chao kisichokuwanamachozi,

Na

UjiangalieMwiliwakounaomeretaujanawaufanisi,

Garilako la kifaharilililozibwavioo,

Jumbalako la kujishashakamauwanjamdogo,

Malaki yapesa unayo miliki,

Ujii tapo mwajiri kwa raha, hunusiusahawa hali yao?

Maswali

(a) Je, mashairi haya mawili niyaa ina gani? Toa sababu. (alama 2)

(b) Taja dhamira kuu katika kila shairi. (alama 2)

(c) Kwa kutoa hoja zozote **tatu** linganua mashairi haya kiumbo. (alama 3)

(d) Taja na uelezee **nafsinenewa** katika mashairi haya mawili. (alama 2)

(e) Kwa kutolea mfano **mmojammoja** eleza matumizi ya mbinu hizi za kimtindo katika shairi la A. (alama 2)

(i) Kweli-kinzani

(ii) Mishata

(f) Tambua **idhini** ya kishairi iliyotumika katika neno "Waichezeye" na uelezee dhima yake katika utoshelezi wa kiarudhi. (alama 1)

(g) Dondoa mfano **mmojammoja** wa mbinu ya tashhisi kutoka kwenye mashairi yote mawili. (alama 2)

(h) Andika ubeti wa **tatu** katika **shairi la A** kwa lugha anathari. (alama 4)

(i) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika vifungu hivi. (alama 2) (i) Inampiku. (ii) Makontena.

3. FASIHI SIMULIZI **ALAMA 20**

i) Umepewa jukumu la kutafiti kuhusu michezo ya watoto katika jamii yako.

a) Taja eneo ambalo utafanyia utafiti wako. (alama 2)

b) Fafanua mbinu ambazo utatumia kukusanyia data huku ukionyesha sababu za

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

uteuziwako. (alama 18)

Au

ii) a) Ni nini maana ya ulumbi (Alama 2) b) Eleza sifa **nne** za mtendaji katika ulumbi (Alama 8)

c) Ngomezi zina majukumu yapi **manne** katika jamii yako? (Alama 8)
d) Toa mifano **miwili** yangomezi katika jamiiyako (Alama 2)

TAMTHILIA: KIGOGO Na Pauline Kea
ALAMA 20

i) "…kulindauhai, kulindahaki, kulindauhuru…"
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
b) Taja nau fafanue maudhu imawili yanayojitokeza katika dondoo hili (alama 4)
c) Msemaji wamaneno hayaa lifanikiwa kulinda uhai, kulinda haki nakulinda uhuru. Dhibitisha kwa kurejelea tamthilia nzima (alama 12)

Au

ii) Fafanua aina zozote kumi za migogoro ijitokezayo katika tamthilia ya kigogo (alama 20)

4. HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE Na Alifa Chokocho Na Dumu Kayanda

ALAMA 20

i) Shibe Inatumaliza- Salma Omar Hamad

"…lakini kulakuna tumaliza vipi?"

a) Eleza muktadha wadondoo hili. (alama 4)
b) Eleza jinsi kulakunavyo tumaliza kwa mujibu wa hadithi. (alama 6)

Mame Bakari-Mohammed Khelef Ghassany

c) Eleza maudhui yafuatayo kama yalivyojitokeza katika hadithi ya Mame Bakari
i) Uwajibikaji (alama 6) ii) Ukatili (alama 4)

Au

ii) Hukuu kirejelea hadithi ya**Tumbo Lisiloshiba** na **Shibe Inatumaliza,**fafanua maudhui ya **ukiukaji wa haki.** (al.20)

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0705525657

FOR MORE ERESOURCES CALL 0705525657